# Nipashe

Alhamisi Machi 4, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580509

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11

**Mahakama** yaamuru vipimo vinasaba padri anayedaiwa kubaka

UKURASA 3



**BoT** yaagiza benki kubana wafanyakazi wanaofanya uhalifu

UKURASA 4



# Kila kona ni kilio umeme

• **TANESCO** yaeleza chanzo, kumaliza ndani ya siku tano... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**SERIKALI YAANDAA MKAKATI UWEKEZAJI**

SERIKALI imesema inaandaa mkakati wa kuinua kiwango cha...

UKURASA WA 5

**PM AAGIZA KUPUNGUZA MUDA MELI ZA MIZIGO**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameiagiza Mamlaka ya...


## Mazrui, Mkuya mawaziri Zanzibar

UKURASA 3



# Vitu hivi kuhatarisha usikivu kwa mamilioni

UKURASA 2





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



MICHEZO GOMES AICHAMBUA AL MERRIKH UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# Kilio umeme kila kona

**Na Waandishi Wetu**

KILIO kila kona. Ndivyo hali ilivyo kutokana na adha ya kukatika umeme kila mahali nchini, hivyo kusababisha wananchi kushindwa kufanya shughuli za maendeleo.

Hali hiyo imekuwapo kwa takriban wiki moja sasa katika maeneo mbalimbali huku viongozi wa serikali akiwamo Waziri wa Nishati, Dk. Merdard Kalemani (pichani), kutaka tatizo hilo limalizike haraka.



Wakati hali ikiwa hivyo, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) limetoa sababu za kukatika kwa umeme na kusema ndani ya siku tano litakuwa limepatiwa ufumbuzi.

Uchungzi uliofanywa na gazeti hili umeonyesha kuwa maeneo mengi ya nchi kuna tatizo hilo ambalo limeathiri kwa kiasi kikubwa utendaji kazi katika sekta za umma na binafsi.

Mkoani Mbeya, baadhi ya wananchi walisema shughuli zao zimesimama kwa saa kadhaa kutokana na kukosekana kwa umeme wa uhakika, hivyo kupata hasara.

Maeneo ambayo wananchi wamekuwa wakilalamikia tatizo hilo mara kwa mara ni wilaya ya Mbarali ambayo inatumia njia ya Kongoro, Chunya na baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Kyela.

Hata hivyo, TANESCO Mkoa wa Mbeya, imekuwa likitoa taarifa mara kwa mara kuhusu kukatika kwa umeme kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo marekebisho ya njia za umeme na hitlafu ya nishati hiyo.

Taarifa ya TANESCO Mkoa iliyowasilishwa kwenye Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) Januari 6, mwaka huu, ilisema shirika hilo limeomba Sh. bilioni 10.2 kwa ajili ya kuendeleza miradi ya umeme ikiwamo kurekebisha miundombinu.

**PWANI**

Mkoani Pwani, wakazi wa maeneo kadhaa hususani Wilaya ya Bagamoyo, wamelalamikia kukatika kwa umeme kila wakati kwa muda mrefu bila taarifa.

Wamesema hali hiyo imekuwa ikiwaathiri kutokana na kusimama kwa shughuli za kiuchumi, zikiwamo za ujasiriamali na za kijamii, hivyo kuitaka TANESCO kuwa na utaratibu wa kutoa taarifa mapema.

Wiki iliyopita maeneo kadhaa ya Kata ya Mapinga yalikosa umeme kwa zaidi ya siku mbili.

**HOFU MWANZA**

Hofu imetanda kwa wafanyabiashara na watumiaji wa umeme katika maeneo mbalimbali jijini Mwanza kutokana na kukatika kwa umeme mara kwa mara bila taarifa yoyote.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, baadhi ya wananchi walisema wanalazimika kutumia njia mbadala kunusuru shughuli zao kukwama ikiwamo kutumia jenereta hali inayoongeza gharama katika uendeshaji.

Mmoja wa wafanyabiashara wa barafu eneo la Kisesa jijini Mwanza, Angel Ben, alisema tatizo la kukatika kwa umeme limeitia dosari biashara yake kwa kuwa barafu zote huyeyuka kila siku umeme unapokatika na kuongeza kuwa hali hiyo imekuwa ikijirudia kwa takriban siku saba sasa.

Nao baadhi ya wananchi katika maeneo mbalimbali Morogoro, wameomba serikali kutafuta ufumbuzi wa kina na wa haraka juu ya ukatikaji wa umeme tangu mwanzoni mwa mwaka huu bila taarifa na wakati mwingine kwa taarifa.

Kwa mujibu wa wananchi hao, hali hiyo inaathiri uzalishaji ambao sehemu kubwa unategemea umeme sambamba na kuharibu vifaa vinavyotumia nishati hiyo.

Baadhi ya wananchi wa maeneo ya Kihonda Mbuyuni, Magorofani, Tushikamane, Mazimbu, Mzumbe, Magadu, SUA na Kasanga, wamelalamikia kukatika huko mara kwa mara kwa umeme bila taarifa na kwamba tatizo hilo limekuwa kero sugu.

Waliomba utatuzi wa haraka na kwamba badala ya TANESCO kusingizia mvua, radi, miti kuangushwa na upepo, ni vyema ikaweka sawa ratiba kama kuna mgawo wa nishati hiyo.

"Mbona zamani hali haikuwa hivi? Hata kama ni dharura hizi zimepitiliza maana imekuwa kila siku, usiku na mchana. Umeme unakatika na muda wa kurudi haujulikani. Nimelazimika kuachana na biashara ya samaki kwani ni hasara tupu. Wanaooza unatupa tu hakuna anayekulipa hiyo hasara," alisema mmoja wa wafanyabiashara wa samaki kutoka Kihonda, Selina Anthony.

Mwananchi mwingine Twaha Burets akabainisha kinachosikitisha ni wakati mwingine umeme kurudi kwa nguvu kubwa na kuharibu soketi za umeme na vifaa vingine vikiwamo friji na televisheni.

Naye Adam Mwansele, mkazi wa Kihonda Maghorofani, alisema kwa takribani wiki sasa, huduma za umeme zimekuwa hazipatikani bila shirika hilo kutoa taarifa yoyote kwa wateja. Alisema hatua hiyo imekuwa ikisababisha usumbufu kwa wakazi wa eneo hilo.

Hassani Kaega, mkazi wa Mazimbu, alisema kukatika kwa umeme katika eneo hilo kumekuwa kukiathiri pia kukosekana kwa maji kwa kuwa maji wanayotumia yanasukumwa na mitambo inayotumia umeme kutoka chanzo cha bwawa la Mindu.

**KILIMANJARO**

Wananchi katika baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Kilimanjaro, wamemtaka Waziri Kalemani kutangaza rasmi mgawo wa umeme lengo likiwa kujipanga namna ya kufanya biashara zao.

Hamis Ramadhani ni kinyozi katika stendi kuu ya mabasi ya Moshi, alisema ni vyema serikali kupitia TANESCO ikatangaza kama kuna mgawo wa umeme na utachukuwa muda gani kuliko kukata umeme kila siku.

"Kwa sasa TANESCO mkoani hapa wanakata umeme hata mara tano kwa siku bila taarifa yoyote na zaidi kabisa hakuna taarifa za ukataji wa umeme huo. Unaweza kukatika hata zaidi ya saa nane," alisema.

Naye Samwel Msuya, mfanyabiashara wa samaki katika soko kuu la kati, Manispaa ya Moshi, alisema kwa takribani mwezi mmoja umeme umekuwa ukikatika kila mara.

"Viongozi wa TANESCO Kilimanjaro si wasikivu na huwatolewa wateja lugha zisizo na staa. Unatoa taarifa ya kukatika kwa umeme hakuna ufuatiliaji. Nimeunguliwa na mafriji mawili na sasa nashindwa kuagiza mzigo wowote kutokana na hali hiyo," alisema Msuya.

**DODOMA SAFI**

Wakati hali ikiwa ya wasiwasi katika mikoa mbalimbali, mkoani Dodoma hakuna mgawo wala tatizo la umeme isipokuwa kumekuwapo na tatizo la kukatika kwa baadhi ya laini kutokana na matengenezo madogo na baadaye umeme hurejeshwa.

Ofisa Habari wa TANESCO Mkoa wa Dodoma, Innocent Lupenza, alisema kwa mkoa huo hakuna tatizo la umeme na kama kuna katizo lolote taarifa hutolewa.

"Hakuna tatizo la umeme kama labda kuna laini umekatika tangazo linatolewa na ni matengenezo ya muda na baadaye kurejeshwa," alisema.

***Imeandikwa na Grace Mwakalinga (MBEYA), Mary Mosha (MOSHI), Idda Mushi na Ashton Balaigwa (MOROGORO) na Elizabeth Faustine (Mwanza).***

## Mamilioni kupata matatizo usikivu

**Na Christina Mwakangale**

MAMILIONI ya watu wako hatarini kupata tatizo la usikivu kutokana na sababu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kiwango cha kelele kwenye maeneo yao ya kazi.

Wataalamu wa afya wamebainisha kuwa asilimia 58 ya wafanyakazi wa viwanda vya nguo wanapata tatizo la usikivu huku matumizi ya pamba za kusafisha masikioni nayo yakichangia ukubwa wa tatizo hilo.

Kundi lingine linalotajwa kuwa hatarini, ni vijana hususan wanaopenda kusikiliza muziki kwa 'earphone' muda mwingi na wanaosikiliza muziki kwa sauti kubwa.

Daktari Bingwa wa Masikio, Pua na Koo (ENT) kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Shabani Mawala, aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya Siku ya Usikivu Duniani.

Dk. Mawala alisema asilimia 58 ya watu wanaofanya shughuli zao kwenye viwanda vya kuchakata nguo, wana tatizo la usikivu kwa kiwango kikubwa.

"Utafiti tulioufanya MNH, unaonyesha asilimia kubwa ya wanaofanya kazi viwandani hasa vya nguo kuliko na kelele na bila kuvaa vizuizi masikioni, wanapata shida hiyo.

"Pia, WHO (Shirika la Afya Duniani) linasema vijana hupoteza usikivu kutokana na kusikiliza muziki. Tatizo lingine la usikivu husababishwa na maambukizi ya virusi na kujaa kwa nta sikioni wananchi wanatumia pamba 'cotton pads' kusafisha masikio ambayo kitaalamu si afya," alisema.

Alisema utafiti unaonyesha zaidi ya asilimia tano ya watu duniani wana tatizo la usikivu, huku mwaka jana watu milioni 466 wakiwa na tatizo hilo na baadhi kupata ulemavu.

"Kati ya hao milioni 466, watoto ni miloni 34. Matumizi mabaya ya dawa baada ya mtoto kuzaliwa, maambukizi ya virusi kutoka kwa mjamzito kwenda kwa mtoto inaweza kuwa sababu.

"Dawa ambazo mama anatumia wakati akiwa mjamzito bila ushauri wa daktari, mtoto baada ya kuzaliwa akikosa oksijeni, inaleta shida katika mishipa ya fahamu atakosa usikivu," alisema.

Dk. Mawala alisema uchunguzi wa mara kwa mara kutambua kiwango cha usikivu unasaidia kupunguza kupata ulemavu wa hali hiyo.

"MNH tuna njia mbalimbali kutoa jawabu za walio na shida ya usikivu, ambao nta imejaa na ambao wanahitaji kupandikizwa kifaa cha usikivu, ila kabla ya kufikia hatua hiyo tujitahidi kujilinda tusipoteze usikivu," alisema.

Alisema mfumo wa usikivu ni kati ya mifumo ya fahamu ya binadamu ambayo hufanya kazi kwa asilimia 100 na kwamba tatizo linapotokea, kuna njia ya kutatuliwa.

"Kwa watu wazima ambao wanapoteza usikivu, sababu ni nta. Kaulimbiu mwaka huu ni 'Afya ya Usikivu kwa Wote, Chunguza, Tengemaza na Watu Waweze Kuwasiliana'," alisema.

# Mazrui, Mkuya wateuliwa mawaziri

Na Mwandishi Wetu

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amefanya uteuzi wa mawaziri wapya wawili katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Katika taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said, ilisema Rais amefanya uteuzi huo kwa mujibu wa mamlaka alipopewa chini ya vifungu vya 42,43 (1)(2) na 44 vya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Taarifa hiyo ilisema walioteuliwa ni Dk. Saada Mkuya Salum ambaye ameteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Wengine walioteuliwa ni Omar Said Shaaban kuwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda na Nassor Ahmed Mazrui ambaye anakuwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, uteuzi huo umeanza jana na wateule hao wataapishwa leo saa 4:00 za asubuhi katika Ukumbi wa Ikulu, Zanzibar.

Sambamba na hao, Rais Mwinyi pia atamwapisha Salum Yussuf Ali, Kamishna wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) ambaye aliteuliwa Februari 10, mwaka huu.



Mkuya



Mazrui



Mwenyekiti wa Chama cha Wanasheria Wanawake nchini (TAWLA), Lulu Ng'wanakilala, amkabidhi tuzo Balozi Mkazi wa Umoja wa Ulaya, Manifredo Fanti, jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni kuthamini mchango wa umoja huo, katika kuwezesha upatikanaji wa haki za wanawake nchini. **HABARI UK. 7.** **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

## Mahakama yaagiza vipimo vya DNA padri anayedaiwa kubaka

**Na Daniel Sabuni,** HAI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Hai imeamuru aliyekuwa Paroko wa Parokia ya Manushi, Jimbo Katoliki la Moshi, Erasmus Swai, kupima vinasaba (DNA) na mtoto wa miezi mitano pamoja na mama yake ili kujiridhisha kuhusu baba wa mtoto huyo.

Kiongozi huyo wa kiroho anadaiwa kumbaka na kumpa ujauzito mama wa mtoto huyo alipokuwa mwanafunzi mwenye miaka 17 katika Shule ya Sekondari Kimaseki mkoani Arusha.

Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Hai, Thurston Kombe, alitoa agizo hilo jana mahakamani huko kutokana na ombi la Upande wa Mashtaka unaongozwa na Mwendesha Mashtaka, Lobulu Mbise.

Katika kesi hiyo namba 6 ya mwaka 2021, Upande wa Mashtaka ulitoa ombi hilo la kupima vinasaba vya watatu hao ili kukamilisha upelelezi wa shauri hilo.

Hakimu Kombe alisema mahakama imeridhia ombi hilo na kuagiza vipimo hivyo kufanyika haraka ili haki itendeke na kubaini kama tuhuma hizo dhidi ya padri huyo ni za kweli au la.

Awali, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Mbise, aliwasilisha maombi hayo kwa mahakama wakati kesi hiyo ilipotajwa ili kukamilisha ushahidi na kesi hiyo ianze kusikilizwa.

Kutokana na amri hiyo, Mwendesha Mashtaka alidai Padri Swai anapaswa kwenda kwa mpelelezi wa kesi hiyo ili apelekwe kwa Mkemia wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa (Mount Meru), ili achukuliwe sampuli pamoja na anayedaiwa kuwa mtoto wake na mama yake.

Kesi hiyo itatajwa tena mahakamani huko Machi 31, mwaka huu.


Tpb Bank
Grow with us

PONGEZI



Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Benki ya TPB Plc inaungana na Watanzania wote kwa ujumla kumpongeza

**Mhe. Othuman Masoud Othuman Sharif**

Kwa kuteuliwa kuwa

Makamu wa kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

www.tpbbank.co.tz | info@tpbbank.co.tz, marketing@tpbbank.co.tz | facebook/tpbbank | 0787 669977

# BoT kuwabana wafanyakazi

**Na Salome Kitomari**

BENKI Kuu (BoT), inakusanya taarifa za wafanyakazi wa benki na taasisi za fedha nchini ili kuhakikisha zinasimamiwa na kuongozwa na wafanyakazi waadilifu wakati wote, na kuzuia kusambaa kwa wasio waadilifu.

Ufafanuzi wa BoT unakuja kutokana na waraka wenye kumbukumbu namba FA 535/01/46 ya Februari 26, mwaka huu, kwenda kwa benki zote, ukizitaka kutoa orodha ya wafanyakazi waliopo na waliokuwapo na kuhusika katika matukio ya utovu wa nidhamu na uhalifu.

"Kwa barua hii benki na taasisi zote za fedha zinatakiwa kuwasilisha taarifa za wafanyakazi waliosimamishwa au wanaotarajia kusimamishwa kwa makosa ya utovu wa nidhamu na uhalifu, na walioacha kazi wakati mashauri ya kinidhamu yanashughulikiwa," ilisema sehemu ya barua hiyo iliyosainiwa na Emmanuel Akaro na Sadati Musa.

Pia barua hiyo imesema kuwa taarifa zinazotakiwa ni za kipindi cha Januari mwaka 2011 hadi sasa na zikusanywe kwa siku 10 tangu kupokelewa kwa barua hiyo.

Kwa mujibu wa barua hiyo, baada ya taarifa hizo utoaji wa taarifa utakuwa unafanyika siku saba tangu kufikiwa uamuzi wa kusitisha mkataba au rufani zozote na kuacha kazi wakati wa mchakato wa hatua za kinidhamu.

Ufafanuzi wa BoT kuhusu suala hilo, uliotolewa na Idara ya Uhusiano wa Umma na Itifaki, ni kutokana na umuhimu wa benki na taasisi za fedha kwa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu, hasa katika utunzaji wa amana za wateja na kuzigawanya katika sekta muhimu za kiuchumi kupitia utoaji mikopo.

"Benki inakusanya taarifa za wafanyakazi wote waliowahi kuachishwa kazi kwa sababu zinazohusiana na uadilifu, lengo ni BoT kuhakikisha wafanyakazi hao waajiriwa katika benki na taasisi za fedha nyingine na kusababisha hasara," ilisema taarifa hiyo na kuongeza:

"Hili litafanywa na BoT kwa umakini na hasa baada ya kujiridhisha kwamba kulikuwa na sababu za msingi za kuachishwa kazi ili kupunguza uwezekano wa uonevu."

Kuhusu kwanini zinatakiwa taarifa za tangu 2011, walifafanua kuwa BoT imegundua makosa ya uadilifu yamekuwa yakifanyika kwa muda mrefu ndani ya taasisi hizo na wafanyakazi waliofanya makosa wamekuwa wakihama kutoka benki au taasisi ya fedha moja kwenda nyingine.

"Hatua mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa na benki moja moja bila kuwapo mawasiliano na benki nyingine, imesababisha baadhi ya wafanyakazi wasio waadilifu kuhama kutoka benki moja hadi nyingine. Kwa kupata taarifa za miaka 10 iliyopita BoT itapata nafasi ya kuwatambua wafanyakazi hao na kuchukua hatua stahiki," ilisema taarifa hiyo.

Aidha, BoT ilisema sababu nyingine ni ongezeko la idadi ya benki pamoja na huduma zinazotolewa na taasisi hizo, hasa za mitandao ya kielektroniki, hali ambayo imeboresha huduma za kibenki na kuongeza changamoto za baadhi ya wafanyakazi kutaka kujinufaisha kwa njia za udanganyifu.

BoT ilisema waraka huo una maana kuwa wafanyakazi wa benki na taasisi za fedha wawe waadilifu kuziendesha na kuzisimamia taasisi hizo katika nyanja zote zikiwamo kulinda amana za wateja na utoaji mikopo.





Wanafunzi wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Atlas Madale, wakiwa kwenye foleni ya kupiga kura kwenye uchaguzi wa viongozi wa serikali ya wanafunzi wa shule hiyo, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Serikali yaandaa mkakati uwekezaji

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema inaandaa mkakati wa kuinua kiwango cha uwekezaji kwenye kila halmashauri nchini.

Imesema mkakati huo mpya utapima kiwango cha mikoa yote katika kuwavutia na kuwahudumia wawekezaji.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Uwekezaji), Prof. Kitila Mkumbo, aliyasema hayo jana mkoani Katavi alipozindua mwongozo wa uwekezaji wa mkoa huo.

Prof. Kitila alisema ni wakati sasa watumishi wa umma kuchukua jukumu lao na kuwawezesha wawekezaji kuwekeza katika mazingira bora na tulivu na siyo kuwekewa vizingiti ama urasimu.

"Ili serikali itoe huduma, ni lazima tuwe na uchumi. Kama unataka serikali ikuhudumie vizuri, ni lazima uheshimu wawekezaji. Serikali itaendelea kuwajali, kuwapatia fursa stahiki wawekezaji, ili kukuza uchumi wa nchi.

"Hoja tunapozungumzia uwekezaji siyo lazima uwe mgeni. Ili kuvutia wawekezaji, ni muhimu sekta binafsi ya ndani na ya nje pamoja na serikali kushirikiana. "Unachukia, unapowanyanyapaa wawekezaji na wakati huohuo unahitaji fedha, siyo sawa," Prof. Mkumbo alisema.

Alibainisha kwamba maofisa biashara walioko katika kila halmashauri, watumike pia katika kusimamia uwekezaji, ili kuinua kiwango cha uwekezaji kwenye maeneo yao.

"Nimeshuhudia shughuli za uwekezaji zinazoendelea katika Mkoa wa Katavi kwenye mazao ya mahindi, mpunga na pamba.

"Mkoa wa Katavi ni muhimu kwa nchi husussan katika kilimo. Katavi ni kati ya mikoa minne bora nchini, pia inasifika kwa kuwa na madini na utalii," alisema.

Prof. Kitila alisema mfumo wa uchumi wowote duniani unategemea vyanzo vingi ikiwamo uwekezaji, maarifa na uzalishaji.

# Lukuvi aamuru kufutwa hati yenye mgogoro miaka 14

**Na Munir Shemweta,** NYAMAGANA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ameamuru kuondolewa katika daftari hati ya kitalu namba 153 na eneo hilo kupatiwa wananchi 74 waliokuwa katika mgogoro katika kata ya Mhandu, Nyamagana mkoani Mwanza.

Akitoa uamuzi huo jana wilayani hapa wakati wa ziara yake kwa ajili ya kutatua mgogoro wa eneo hilo uliodumu kwa takriban miaka 14, Lukuvi alisema hati ya mtu anayedaiwa mmiliki wa eneo hilo anayetambulika kwa jina la Abdallah Maliki, ilitakiwa kufutwa muda mrefu kwa kuwa hajalipia kodi ya pango la ardhi kwa miaka 15.

"Hati miliki ikaondolewe katika daftari la hati na jaji amethibitisha katika uamuzi wake kuwa wamiliki wa asili katika eneo hili hawakulipwa fidia," alisema Lukuvi.

Waziri aliongeza kuwa kutokana na uamuzi huo, sasa wananchi wa eneo hilo watatakiwa kupimiwa kulingana na ukubwa wa eneo analomiliki na kila mmiliki atatakiwa kulipa tozo ya mbele asilimia 2.5 kufidia gharama ambayo mmiliki wa awali alishindwa kulipa kodi ya pango.

"Huyu mtu ameshindwa kuendeleza kwa wakati na hajalipa kodi kwa miaka 15. Sasa wananchi wapimiwe na kupatiwa eneo bila fidia. Huwezi kupewa eneo una hati watu 70 wanajenga miaka 15 wewe una hati umekaa nayo tu," alisema Lukuvi.

Kwa mujibu wa Lukuvi, serikali itahakikisha inalinda hati ya mmiliki wa ardhi huku mmiliki akitakiwa kulinda eneo lake na kusisitiza kuwa hati ya ardhi ni dhamana na ndiyo inayotoa usalama wa mmiliki.

"Mtu hajaonekana halafu atoe kibali cha kuvunja nyumba. Sheria hairuhusu umilikishaji juu ya hati nyingine ndiyo maana nimeamua kuifuta kwanza hati hii ndiyo hati nyingine isajiliwe," alisema.

Pia aliagiza eneo lingine kitalu Na. 154 linalokaliwa na wananchi 40 na kumilikiwa na Abdulkarim Mbaga, mmiliki wake apelekewe ilani ya siku 90 kabla ya hatua za kisheria hazijachukuliwa dhidi ya eneo lake.

Akiwasilisha mgogoro huo mbele ya Waziri, mwakilishi wa wananchi wa Kata ya Mhandu Sokoni, Kazimiri Shimbi, alisema muda mrefu wananchi wa eneo hilo wamekuwa katika mgogoro wa ardhi wakishtakiwa na mtu wasiyemjua jambo lililosababisha kushindwa kurasimishiwa makazi katika eneo hilo kwa madai ya kuvamia eneo.

Kwa mujibu wa Shimbi, wananchi hao mara kadhaa wamekuwa wakishinda kesi mahakamani dhidi ya mdai.

## HABARI KITAIFA

# PM aagiza kupunguza muda meli za mizigo

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameiagiza Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), kuangalia uwezekano wa kupunguza muda wa meli zinazoshusha mzigo bandarini.

Alitoa agizo hilo jana, alipofanya ziara katika Bandari ya Dar es Salaam.

Alisema pamoja na hatua nzuri iliyofikiwa na TPA kupunguza muda mwingi uliokuwa ukitumika kwa meli hizo kushuka mzigo, pia inapaswa kuangalia pia kupunguza zaidi ili kuwe na idadi kubwa ya meli zinazoingia bandarini.

"Awali meli zilikuwa zinatumia siku 15 kushusha mzigo, lakini kwa TPA mmefanya kazi kubwa kupunguza muda huo na hii ni improvement (mabadiliko) kubwa sana, lakini tuendelee kuona uwezekano wa kupunguza siku zaidi angalau zifike nne au tano na wataalamu wa mitambo tunaomba muone namna ya kutufikisha hapo, tunataka meli ishuke lita zake zote 100,000 kwa siku nne halafu iingie nyingine ili tuwe na flow kubwa ya meli zinazoingia," alisema Majaliwa.

Alitaka pia maboresho yanayofanywa na TPA kwenye bandari hizo yasaidie kuondoa tatizo la msongamano wa meli hizo.

"Tulishaagiza kazi ifanyike saa 24, tunataka hata maofisa wanaotakiwa kufanya kazi saa 24 waje wafanye kazi ili tupunguze msongamano wa meli na kwa njia hiyo zitaingia nyingi zaidi na tutashawishi wenye kampuni za meli kuja hapa, Bandari ya Mtwara na Tanga na mapato yataongezeka zaidi," alisema Majaliwa.

Pia alisema serikali haitakuwa na watendaji wanaochangia kupoteza mapato na kila watakapokuwa wanabainika wa namna hiyo watakuwa wanaendelea kuwachukulia hatua.

"Hapa ndio chanzo cha mapato yetu na tunatamani mnayopata sasa yaongezeke zaidi, hatutakubali kuwa na watu wanaochangia kupoteza mapato iwe Dar es Salaam, Mtwara au Tanga tunataka kile kinachoingia kikafanye maendeleo ya nchi, hayo ndiyo malengo yetu na wale watakaobainika kupoteza mapato tutakuwa tunawachunguza na kuwachukulia hatua," alisema Majaliwa.

Aliiagiza TPA kuimarisha taasisi ambayo itahusika na kusimamia ujenzi wa mitambo na mifumo ya mafuta katika bandari zote za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga.

"Kuna umuhimu mkubwa kwa TPA kuimarisha taasisi ambayo itakuwa inasimamia hii mifumo ya mafuta (Flow meter), tulipokaa pamoja tulikubaliana tuwe na idara maalum inayoshughulikia flow meter zote za Bandari ya Dar es Salaam, Mtwara na Tanga, wao wawajibike kwenye utunzaji, utoaji wa huduma hiyo, lakini pia kama kunakuwa na jambo lolote linalolalamikiwa wao ndio watawajibika kutuambia ni nini kilitokea, kukiwa na mamlaka hiyo kazi itaenda vizuri," alisema Majaliwa.

Hatua ninayoiona leo ya watendaji wetu wa bandari kusimamia hizi mita ni nzuri, lakini tunachokihitaji sasa wale wataalam wetu walioko kwenye mifumo hii wale waaminifu, ikiguswa inaharibu maeneo mengi, kwa hiyo ni muhimu tuwe na watu wenye mapenzi na jambo tunalolifanya ndani ya nchi kwa manufaa ya Tanzania.

# Waziri Aweso aiwakia DDCA

**Na Frank Monyo**

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, ametoa siku saba kwa Wakala wa Uchimbaji Visima na Mabwawa (DDCA) kurejesha mitambo minne ya uchimbaji mabwawa wizarani na ikigundulika kuna ujanja umefanyika, hatua kali zitachukuliwa.

Vilevile, amechukizwa na kitendo cha Mhandisi Mkuu wa Kitengo cha Uchimbaji Mabwawa, Muliani Mugaiwa, kumdanganya kuhusu ziliko mashine hizo akidai zipo karakana ilhali si kweli.

Alitoa agizo hilo jana Dar es Salaam wakati wa ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa DDCA na kukagua mitambo ya wakala huo.

"Ninataka mnionyeshe vifaa vya upimaji, wala hakuna majadiliano, wewe si ndiyo mtendaji wa hapa? Twende ukanionyeshe vifaa kwani kuna tatizo gani? Twendeni stoo mnapodai ipo mitambo," alisema.

Baada ya kufika kwenye karakana ya DDCA iliyoko Wizara ya Maji eneo la Ubungo na kukosa mitambo hiyo kwa maelezo kuwa ilikuwa kwenye eneo la kazi, Aweso alihoji sababu za kutorejeshwa ilhali kazi imesimama.

Alisema kuwa anafahamu kuwa mitambo hiyo imezuiwa kwa sababu kazi hawakumaliza na pesa walizopewa DDCA wamezila.

"Ninajua kila kitu, wala hakuna cha kujitetea, ndiyo maana mimi nimekuja kuwaeleza, hatuwezi kulalamika kwamba ninyi mna mitambo na haifanyi kazi.

"Menejimenti ya kusimamia visima haifanyi sawa, mtu wa 'private' anafanya kazi kwa siku tano amekamilisha, lakini nyie mnafanya miezi miwili, ili mradi tu mpate posho ambazo hazina ulazima wowote.

"Sasa nawaambia DDCA mjipange, na msipojipanga mimi nitawasaidia kuwapanga, haiwezekani kunidanganya eti mitambo ipo stoo, ninakwambia nionyeshe hakuna.

"Mtumishi wa umma unakuwa muongo muongo, mimi ninafahamu ... (anataja jina) amehujumu mitambo hiyo minne haifanyi kazi, inakuwaje yeye mitambo yake inafanya kazi lakini ya serikali haifanyi kazi? Nilimfukuza kazi," alisema.

# NOTISI/ TANGAZO

**NUTMEG AUCTIONEERS AND PROPERTY MANAGERS CO.LTD, MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTOR LTD, TAUSI AUCTION MART CHAMPION AUCTION MART LTD, SUNDI AUCTION MART LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, , BEST GROUP LTD, , SALEI AUCTION MART LTD** kwa mamlaka tuliyo pewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tuna toa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili,Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| S/No | JINA LA MTEJA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | HAJI HARAMBE BIBOZE | HAJI HARAMBE BIBOZE NA IBRAHIM RASHIDI IBRAHIM | NYUMBA | VIKINDU NA TUONGOMA | 19/03/2021 NA KUENDELEA |
| 2. | HY- LINE INVESTMENT | GOFREY HILLDEPHONE BAITWA | NYUMBA | MTAA WA MACHINJIONI (KWA MBIKU) KATA YA MIANZINI | 23/03/2021 NA KUENDELEA |
| 3. | EDWIN AUGOSTINO MASENYA | EDWIN AUGOSTINO MASENYA | NYUMBA | MAJOHE (MOSHI BAR) KIPUNGUNI B- | 26/03/2021 NA KUENDELEA |
| 4 | REHEMA JABIL MUTASHUBILWA | REHEMA KAGEMULO MUTASHUBILWA | NYUMBA | MAJOHE – GONGO LA MBOTO (ILALA) | 23/03/2021 NA KUENDELEA |
| 5 | ABINERI MESHACK SANGE | ABINERI MESHACK SANGE | NYUMBA | BAGAMOYO-NIA NJEMA | 16/03/2021 NA KUENDELEA |
| 6 | ELIUD SIMON MHEMBU | ELIUD SIMON MHEMBU | NYUMBA | KINZUDI-GOBA | 20/03/2021 NA KUENDELEA |
| 7 | FREDRICK BALTAZARY PETER | FREDRICK BALTAZARY PETER | NYUMBA | ULONGONI 'B' | 23/03/2021 NA KUENDELEA |
| 8 | MUSA NG'OMBE NKOBA | ZUHURA ISSA FERUZI | NYUMBA | MWONGOZO - TABATA | 26/03/2021 NA KUENDELEA |
| 9 | JAMIMA PAUL SELEMANI | MARCO MWITA MARCO | NYUMBA | TOANGOMA-KIGAMBONI | 29/03/2021 NA KUENDELEA |
| 10 | REGINA CHARLES KAJOLE | ATHUMANI RAJABU JONGO | NYUMBA | KILUNGULE-MBAGALA | 07/04/2021 NA KUENDELEA |
| 11 | TAMIKA IZACK MWALUMU | TAMIKA IZACK MWALUMU | NYUMBA | KINYEREZI- KIBAGA | 03/04/2021 NA KUENDELEA |
| 12 | PRISCA CLEMENT KAGORO | NESTORY ISDORY WANGA | PLOT NO.774 BLOCK ' P' | BUHONGWA-MWANZA | 19/03/2021 NA KUENDELEA |
| 13 | EDMUND KAJUNGU MENDRAD | EDMUND KAJUNGU MENDRAD | PLOT NO1237 BLOCK :LL: | KILOLELI-MWANZA | 20/03/2021 NA KUENDELEA |
| 14 | JOSEPH MAIRO GETERE | CHACHA MSENYE CHACHA | PLOT NO.27,BLOCK B | NYAMHONGOLO-MWANZA | 20/03/2021 NA KUENDELEA |
| 15 | STEPHANO KUNYA CHAMA | STEPHANO KUNYA CHAMA | NYUMBA | MATALE/SAMBAGULI/BUJASHI | 18/3/2021 NA KUENDELEA |
| 16 | PAUL GEORGE MSEMA | PAUL GEORGE MSEMA | NYUMBA | ILENDEJA/BUJASHI | 19/03/2021 NA KUENDELEA |
| 17 | RWEYEMAMU MENDRAD KABENDERA | RWEYEMAMU MENDRAD KABENDERA | NYUMBA | NYASHISHI | 24/03/2021 NAKUENDELEA |
| 18 | ZUHURA IBRAHIMU GIWANA | ZUHURA IBRAHIMU GIWANA | NYUMBA | KATA YA DARAJA MBILI MTAA WA ALINYANYA - ARUSHA | 19/03/2021 NA KUENDELEA |
| 19 | FRANK PAUL ROIKA | FRANK PAUL ROIKA | NYUMBA | KIJIJI CHA ENGORIKA KATA YA KIUTU-ARUSHA | 20/03/2021 NA KUENDELEA |
| 20 | ISACK BALTAZAR MMASY | ISACK BALTAZAR MMASY | KIWANJA | KATA YA TERATI MTAA WA BONDENI KATI-ARUSHA | 19/03/2021 NA KUENDELEA |
| 21 | MASANJA JAMES WANNA | MASANJA JAMES WANNA | KIWANJA NA MASHINE ZA KUTOTOLEA VIFARANGA 2 | KATA YA TERATI MTAA WA BONDENI KATI-ARUSHA | 20/03/2021 NA KUENDELEA |
| 22 | ARSEN LEONARD SHIRIMA | ARSEN LEONARD SHIRIMA | KIWANJA NO 1 KISALE | WILAYA YA ROMBO | 22/03/2021 NA KUENDELEA |
| 23 | ARSEN LEORNAD SHIRIMA | ARSEN LEONARD SHIRIMA | NYUMBA | KATA YA DARAJA MBILI MTAA WA KATI ARUSHA | 22/03/2021 NA KUENDELEA |
| 24 | ENOS RUBEN SILAA | ENOS RUBEN SILAA | NYUMBA | KATA YA LEMARA MTAA WA ILKIROWA-ARUSHA | 22/03/2021 NA KUENDELEA |
| 25 | BARAKAEL KUNDANDUMI MBISE | BARAKAEL KUNDANDUMI MBISE | NYUMBA | KIJIJI CHA KING'ORI-ARUSHA | 23/03/2021 NA KUENDELEA |
| 26 | MELCKZEDECK EXAUD MBISE | MELCKZEDECK EXAUD MBISE | NYUMBA | KIJIJI CHA KIMUNDO-ARUSHA | 23/03/2021 NA KUENDELEA |
| 27 | MWAMPYATE LEONARD EDWIN | MWAMPYATE LEONARD EDWIN | NYUMBA | KONGOLOMKOLO – MSWISWI-MBEYA | 20/03/2021 NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. **0754497396 /0765999000/0719351040**
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Pongezi kwa madarasa ya ziada, uhaba uwe historia*

**FEBRUARI** 28, mwaka huu, ilikuwa siku ya mwisho kwa wakuu wa mikoa nchini kutekeleza agizo la serikali la Desemba mwaka jana, kujenga madarasa ili kuwachukua wanafunzi 74,166 waliokosa nafasi za kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu licha ya kufaulu.

Juzi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ilitoa taarifa ya utekelezaji wa agizo hilo ikibainisha kuwa vyumba vya madarasa 2,257 vimejengwa ndani ya miezi miwili.

Madarasa yaliyohitajika kwa ajili ya wanafunzi hao ni 1,484, hivyo ujenzi wa vyumba 2,257 umeifanya nchi kuwa na ziada ya madarasa 773 yanayotosha kuchukua wanafunzi 38,684 kwa uwiano wa 1:50.

Nipashe tunaipongeza serikali kwa utekelezaji wa mradi huo wa dharura na kuwanusuru wanafunzi hao maelfu kukosa haki yao ya kupata elimu.

Kimsingi, uhaba wa madarasa ambao umejitokeza wakati wa udahili wa wanafunzi wa kidato cha kwanza kwa miaka mitatu mfululizo, umetokana na ongezeko la wanafunzi wanaodahiliwa kujiunga na elimu ya msingi sambamba na kutotekelezwa kikamilifu kwa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG).

Katika ripoti yake kuhusu Ukaguzi Maalum wa Miundombinu ya Shule za Msingi iliyowasilishwa bungeni Aprili 13, 2017, CAG (kipindi hicho Profesa Mussa Assad), alisema amebaini udahili wa wanafunzi katika shule za msingi nchini uliongezeka kutoka wanafunzi milioni 4.8 mwaka 2001 hadi milioni 8.34 mwaka 2016.

Wakati idadi ya wanafunzi kwenye shule za msingi nchini ikiwa ni milioni 8.34 kwa shule za serikali, CAG alibaini kulikuwa na madarasa 108,448 badala ya 208,540, sawa na wastani wa wanafunzi 77 badala ya 45 katika darasa moja inavyotakiwa kisera.

Alifafanua kuwa mwaka 2012, wanafunzi milioni 3.53 walidahiliwa kujiunga na shule za msingi ambazo hazikuwa na madarasa na utaratibu huo uliendelea katika miaka iliyofuata kukiwa na ongezeko hilo la wastani wa asilimia tano kwenye udahili kwa miaka mitano mfululizo.

Ongezeko hilo la wanafunzi katika shule za msingi linaakisi kinachojitokeza sasa sekondari, uhaba wa madarasa.

Katika mapendekezo yake, CAG aliishauri serikali kuimarisha miundombinu kwa kufanya ukarabati kwa majengo yaliyopo na kujenga mapya.


Vilevile, Mei 22, 2017, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, iliwasilisha taarifa bungeni ikibainisha kuwapo upungufu wa vyumba vya madarasa 146,106 katika shule za msingi na vyumba 12,568 sekondari.

Tunaipongeza serikali kwa ujenzi wa madarasa mapya ndani ya muda mfupi, lakini tunaikumbusha kutekeleza mapendekezo ya CAG kuhusu miundombinu ya shule, tukiamini kufanya hivyo kutaligeuza tatizo la uhaba wa madarasa kuwa historia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# *Sukari tamu, lakini kwa mtindo huu ni hatari*

**BILA** shaka, iko dhahiri kuhusu utamu wa sukari na ndio maana imefika mbali kutungiwa methali.

Pia ni miongoni mwa bidhaa muhimu zinazotumika kwa wingi kila siku majumbani, iwe ni kuweka katika chai, uji, juisi na mengineyo.

Hata hivyo, kurejea katika methali 'kizuri hakikosi kasoro.' Sukari hiyo hiyo, pia inatajwa na wataalamu wa miili yetu, kuwa kiamu hicho kina hatari pale inapotumiwa kwa wingi kupita kiasi, angalizo linalosimama hapo ni kwamba, vyema kumuacha mtumiaji akiwa na afya njema.

Wataalamu wa afya wanaweka wazi kuwa kiwango cha sukari tunachotakiwa kutumika katika vinywaji kuanzia chai, uji, juisi na vingine, ni kiasi kidogo, ingawa kinaweza kisiongeze ladha kwa namna inavyotakiwa.

Katika mazingira kama hayo ya ladha kutokolea namna tunavyotaka, baadhi ya watu hupuuzia angalizo na kuamua kukoleza na wanywaji wanajikuta kuangukia katika matatizo mengine makubwa ya kiafya, bila ya wao kujua mzizi wake ni sukari wanayotumia.

Ukumbusho wa jumla wa kitaalamu ni kwamba, katika afya zetu ziada ya sukari inatuzalishia madhara mengi kama vile kudhoofika kwa mfumo wa kinga ya mwili na viungo vyetu, pia ngozi, huku ikiwa na nafasi ya kumsababisha mtumiaji unene wa kupindukia.

Vilevile, wataalamu wa afya wanashauri watu kujiepusha na unywaji juisi na soda kwa wingi, kwa kuwa inaongezea sukari ya ziada. Chupa moja ya soda, inaelezwa kuwa huwa na wastani wa vijiko sita vya sukari.

Daktari Bingwa wa magonjwa ya binadamu, Nzobendo Lucas, kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili, anasema, kinga ya mwili ni silaha ya asili ya kupambana na maambukizo yote yanayosababishwa na bakteria na virusi wengine.

Hivyo, anasema ili mtu kuwa na kinga ya uhakika mwilini, ni muhimu kuiimarisha kwa kutumia vyakula vyenye virutubisho na kujiepusha na ulaji vyakula kama sukari ambazo zinaathiri mfumo mzima wa kinga ya mwili.

Ufafanuzi uliopo ni kwamba, kiasi kikubwa cha sukari kinapoingia kwenye mishipa ya damu, kina kawaida ya kudhoofisha uwezo wa chembehai hizo katika kupambana na bakteria na virusi wanaoweza kuuvamia mwili.

Muungwana naunga mkono ushauri wa daktari huyo, kwani kwa kuzingatia kuwa kinga ya mwili ndiyo msingi wa afya ya binadamu. Basi, ni vyema kila mmoja wetu akajiepusha na matumizi ya vyakula vinavyohatarisha kinga zilizopo mwilini.

Pia niseme kwamba, ni wakati wa kila mmoja wetu akajiuliza na kuchukua tahadhari hasa kuhusu jinsi ambavyo anatumia sukari, je, ni kile kiwango kinachoshauriwa kitaalamu au ambacho kinaweza kinanafasi fulani kuhatarisha afya yake?

Ingawa si rahisi kujiepusha na matumizi ya sukari na kuiondoa katika milo ya kila siku kwa kuwa nayo ina nafasi kubwa katika kuleta afya yake, bado kuna haja ya kuchukuliwa hatua za tahadhari kupunguza matumizi makubwa yaliyopo kwingi.

Uelewa wa madhara ya matumizi makubwa ya sukari, unaweza kumsaidia mtu kupunguza kiwango anachotumia kwa siku na hatimaye kuendelea kuwa na afya njema ambayo kimsingi ni muhimu zaidi. Njia nzuri inayopaswa kufuatwa ni kuachana na mazoea ya kila siku ya kutaka kusikilizia utamu wake kama kwenye chai au uji, badala yake kinachotakiwa ni kuzingatia maelekezo ya kitaalamu kuhusu kiasi cha sukari kinachotakiwa kuwamo katika mlo.

Maelekezo ya kuzingatiwa yanapaswa kuchukuliwa kwenye vinywaji kama juisi. Kwa mlo wa kukunua au uliomo ndani ya vifungashio, kunapaswa kuchunguzwa kiasi cha sukari kilichomo ambacho kinaandikwa nje ya kasha, ili kutambua ama kinafaa au la, hatari kwa afya yako.

Kwa mfano, Dk. Nzobendo anasema, mara nyingi kiasi cha sukari kinachowekwa kwenye kinywaji huonyeshwa kwa gramu na anamaanisha kwamba, kila gramu nne za sukari, ni sawa na kijiko kimoja kidogo.

Anasema, iwapo kinywaji au chakula ambacho mtu anakula kina uzito wa gramu 16 za sukari, hiyo ni sawa na vijiko vidogo vinne.

Kuna vinywaji vingine havionyeshi jina la sukari moja kwa moja na kuwapa ugumu wa uelewa kwa wanywaji.

HABARI KITAIFA

# EU yapewa tuzo haki za wanawake, watoto

**Na Salome Kitomari**

CHAMA cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA), kimetoa tuzo maalum kwa Umoja wa Ulaya (EU) kwa jitihada za kupambana na upatikanaji haki za wanawake na watoto.

Akikabidhi tuzo hiyo jana nyumbani kwa Balozi huyo jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa TAWLA, Lulu Ng'wanakilala, alisema nchi wanachama wa EU kama Denmark, Finland na Sweden, zimekuwa zikitoa fedha na namna nyingine upatikanaji haki za wanawake na watoto kwa miaka 30.

Aidha, alimkabidhi tuzo na machapisho mbalimbali yaliyotolewa na TAWLA ambayo yamekuwa msaada mkubwa katika upatikanaji wa haki za wanawake na watoto, na kwamba anatambua mchango wao, na ndiyo maana katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake wanatoa tuzo hiyo kama kumbukumbu.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo hiyo, Balozi wa EU, Manfredo Fanti, aliishukuru TAWLA na kusema kubadili mtazamo wa jamii katika mila mbalimbali inachukua muda na kwamba wataendelea kusaidia masuala ya usawa wa kijinsia na haki mbalimbali.

"Tunahakikisha wanawake na watoto wanazifikia huduma za kisheria kwa haraka, tuna miradi mingine ambayo siyo ya wanawake na wototo, lakini inagusa maisha yao moja kwa moja bali ina matokeo chanya kwenye maisha yao," alisema.

Kwa mujibu wa Balozi Fanti, wataendelea kusaidia jitihada za kupambana na ukeketaji, na ukatili wa kujinsia ambao umekuwa kikwazo kwa maendeleo ya wanawake na watoto.

Alisema katika kupambana na vitendo hivyo EU imekuja na khanga zenye maandishi 'Maendeleo ya mwanamke ni faida kwa jamii nzima'.

Naye Mkurugenzi wa TAWLA, Tike Mwambipile, alisema kwa miaka 30 wamewafikia wahitaji zaidi ya milioni 10, na kwamba wanaendela kuwafikia wahitaji wengi.

Aidha, alisema walifanikiwa kuwezesha mabadiliko ya sheria kandamizi, kama mabadiliko ya Sheria ya Ardhi miaka ya 90 ambayo imeruhusu wanawake kumiliki ardhi, pamoja na marekebisho ya sheria ya mtoto.

Pia alisema jitihada zinafanyika kuwawezesha wanawake kushiriki nafasi za maamuzi na uongozi kwa ujumla ili kuondoa tofauti iliyopo.

"Licha ya jitihada hizo msaada wa kisheria bado unahitajika kwa kuwa matukio ya ukatili wa kijinsia yanaendelea," alisema Mwambipile.




Kaimu Mkurugenzi wa Benki ya ACB, Juliana Swai (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu benki hiyo kuwa na ubia wa kimkakati na Benki ya Taifa ya Malawi, ambayo imewekeza kiasi cha Sh. bilioni 17. Kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko wa benki hiyo, Dora Saria Kessy. **MPIGAPICHA WETU**

## Waziri ajivunia ubora wa hifadhi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

HIFADHI za Taifa ya Serengeti, Kilimanjaro na Tarangile zimeshinda tuzo za ubora kwa mwaka 2021 zilizotolewa na Jukwaa la Wasafiri Washauri Ulimwenguni (TripAdvisor Travelers Choice Awards 2021).

Akitangaza ushindi huo kwa waandishi wa habari wa Mkoa wa Morogoro jana, Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, alisema Hifadhi ya Serengeti ndiyo imeibuka ya kwanza kati ya hifadhi 25 zilizoshindanishwa duniani kutokana na upekee wa uhamaji wa wanyamapori aina ya nyumbu na ubora wa tambarare isiyo na kikomo.

Waziri Ndumbaro alisema Hifadhi ya Taifa Tarangire yenye sifa ya kuwa na makundi ya tembo na Kilimanjaro ina mlima mrefu katika Bara la Afrika kutokana na kutunza ikolojia mbalimbali za wanyama na misitu ya asili ambayo mingine haipatikani popote duniani.

Alisema tuzo hizo hupatikana kulingana na ubora wa hifadhi, idadi ya mamilioni ya watazamaji, maoni ya wasafiri na makadirio yanayokusanywa kwenye taasisi hiyo kwa mwaka ambapo Tanzania imeshinda tuzo hizo tatu.

Akizungumzia ushindi huo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Allan Kijazi, alisema mafanikio hayo yametokana na Shirika la Hafadhi za Taifa (TANAPA), kufanya jitihada za kuhifadhi uasili wa ikolojia ya viumbehai hao pamoja na misitu ya asili ambayo imekuwa ikisaidia uhai wa wanyama hao.

# LATRA yazindua rasmi tiketi mtandao

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini (LATRA), imezindua rasmi mfumo wa ukataji wa tiketi kwa njia ya mtandao kwa mabasi yaendayo mikoani iitwayo 'Tiketi Mtandao'.

Kupitia mfumo huo mpya, msafiri atatumia simu yake ya mkononi kununua tiketi ya basi na wale wasio na simu wataendelea kutumia mfumo wa zamani kwa kwenda kwenye vituo vya mabasi kupata tiketi kwa mashine za elektroniki.

Baada ya kuzindua huduma hiyo jana, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Gilliard Ngewe, alisema safari ya kufikia matumizi ya mtandao haikuwa rahisi kwa kuwa baadhi ya watu walikwenda mahakamani wakipinga mfumo huo.

Alisema wazo la kuanzisha mpango huo ulianza tangu mwaka 2014, lakini walikutana na changamoto mbalimbali hali iliyosababisha mchakato huo kuchukua muda mrefu kukamilika.

Ngewe alisema mpaka sasa mabasi mengi yameshaunganishwa na mfumo huo na wananchi wanaweza kuanza kununua tiketi zao kwa kutumia 'Application' ya tiketi mtandao kwenye simu zao za mkononi.

Alisema mamlaka hiyo iliamua kuja na wazo hilo ili kuwakomboa wenye mabasi ambao wamekuwa wakifanya biashara kwa muda mrefu, lakini fedha zao zikiishia mikononi mwa watu wengine, hivyo utaratibu mpya utawaongezea mapato.

"Kuna sehemu nchi hii bado hawana usafiri kabisa. Ukienda Liwale, Itigi - Chunya, Mpanda - Kigoma utakuta watu wanatembea muda mrefu kutafuta usafiri na wengine wanapanda magari ya mizigo. Sasa tulijiuliza mbona hali iko hivi, tukagundua kuwa wenye mabasi hawakui na kuongeza mabasi kwa sababu mapato yao yanavuja," alisema.

"Tuliamua kwa dhati kwamba ifike mahali wenye mabasi wafanye biashara yao kwa kujiamini kwamba wataweka hela zao na watapata faida na kuongeza mabasi lakini hivyo leo hii ni furaha kubwa kuona mpango huu umefanikiwa," aliongeza.

Pia alisema kupitia mfumo huo mtu anaweza kumkatia tiketi kwa simu ndugu yake aliyeko kijijini, hivyo kuokoa muda ambao umekuwa ukitumika kufika kwenye vituo vya mabasi.

Kwa mujibu wa Ngewe, mfumo huo mpya si mgeni kwa kuwa unatumiwa na mataifa mbalimbali duniani na una faida nyingi ikiwamo kuwa na uhakika wa taarifa za kutosha kuhusu abiria na biashara nzima ya usafirishaji.

Mwenyekiti wa Bodi ya LATRA, Henry Bantu, alisema miaka ya nyuma kulikuwa na kampuni kubwa za usafirishaji, lakini zilikufa kutokana na kukosekana usimamizi mzuri ili zipate faida na kukua.

Alisema kwa sababu LATRA ipo, haitakubali kuona kampuni za mabasi zinakufa kwa kushindwa kupata faida ndiyo maana imeanzisha mfumo huo ili kulinda mapato yao, ili yasitokee yaliyowahi kutokea huko nyuma.

Pia alisema lengo la LATRA ni kuiboresha na kuiimarisha sekta ya usafirishaji ili wenye mabasi wawe na uhakika na biashara yao na kuondoa mianya ya kuvuja kwa mapato yao.

"Unakuta mtu kakopa basi limpe faida lakini kutokana na mlolongo wa watu aliowaajiri kama dereva, kondakta, fundi anajikuta anamzigo mkubwa hivyo lazima awekewe mfumo utakaomwezesha kurejesha uwekezaji wake na kupata faida," alisema.

# Waonywa kutofanyia anasa fedha za TASAF

**Na Marco Maduhu,** BARIADI

WALENGWA wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wameonywa kuzitumia fedha wanazopewa kwa mambo ya anasa, badala yake wazitumie kujikwamua kiuchumi.

Mmoja wa walengwa wa mpango huo kutoka kijiji cha Ipililo, Wilaya ya Maswa, Naomi Machibya, alitoa ushauri huo juzi wakati maofisa TASAF kutoka makao makuu, walipotembelea walengwa ili kuona maendeleo yao.

Alisema walengwa wa mpango huo wanapaswa kutambua fedha ambazo wanapewa ni za kujikwamua kiuchumi na si kuzifanyia anasa ikiwamo kufanya sherehe na kuzinywea pombe.

"Natoa wito kwa walengwa wenzangu tuzitumie fedha hizi za ruzuku kuwekeza kwenye uzalishaji ikiwamo ufugaji na kilimo na si kuzifanyia anasa. Tukifanya hivyo hatutatoka kwenye umaskini," alisema Machibya.

"Mfano mimi baada ya kupata fedha hizi niliwekeza kwenye kilimo cha mpunga na sasa nimejenga nyumba ya kisasa kabisa na kutoka kwenye nyumba ya tembe. Pia nina kuku 30 na sasa si maskini tena," aliongeza.

Mlengwa mwingine, Njile Malambi, alisema baada ya kuanza kupokea fedha za mpango huo, alianza kununua kuku, kisha akawauza akanunua mbuzi nao akawauza na kununua ng'ombe na sasa ana ng'ombe watatu wa maziwa.

Mratibu wa TASAF Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, Grace Tungaraza, alisema kabla ya kuwapatia fedha walengwa hao, wanawapatia kwanza elimu ya matumizi sahihi ili wajikwamue kiuchumi ikiwamo kujikita kwenye ufugaji na kilimo.

Alisema asilimia 80 ya walengwa wa TASAF wilayani humo maisha yao yamebadilika, tofauti na awali.

Mkoa wa Simiyu una walengwa 8,836 na kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka jana, jumla ya Sh. bilioni 5.7 zimeshatolewa kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi.




Mkuu wa Idara ya M-Pesa Biashara, Happiness Shuma, akizungumza wakati wa uzinduzi wa mfumo wa ukataji wa tiketi kwa njia ya mtandao kwa mabasi yaendayo mikoani uitwao 'Tiketi Mtandao', uliondaliwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), jijini Dar es Salaam jana, utakaowezesha wasafiri kulipia nauli kupitia simu za mkononi, huduma za kifedha za benki kwa kuingia kwenye App ya Tiketi Mtandao na menu ya M-Pesa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## RC awanusuru mabinti kuolewa

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, amewakamata wanafunzi sita wa jamii ya wafugaji, ambao walikuwa wamefikishwa kwa madai ya kutaka kuozeshwa, baada ya kuhitimu darasa la saba na kufaulu vizuri.

Msako huo ulifanyika juzi baada ya Ole Sanare aliyeambatana na kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa huo, kubaini hilo na kuamua kwenda kitou cha shule cha Ngunya walipokuwa wanafunzi hao.

Ilielezwa kuwa wanafunzi hao sita baada ya kuhitimu elimu ya msingi na kufaulu kijiunga na kidato cha kwanza, wazazi wao wanaioshi wilayani Kilosa waliwatafuta wanaume na kutaka kuwaoza ili wapate ng'ombe.

Kwa mujibu wa Diwani wa Kata ya Parakuyo, ambako wazazi wa wanafunzi hao wanaishi, Ibrahimu Kalaita, alisema mabinti hao walihitimu darasa la saba mwaka jana na walifaulu kisha kuchaguliwa kijiunga ya Shule ya Sendondari Parakuyo.

"Baada ya kuhitimu na kufaulu mtihani wa darasa la saba mabinti hawa hawakujiunga na shule waliyokuwa wamechakuliwa kwani wazazi wao waliwatafutia wanaume kuwaozesha ili wapate mali," alisema Kalaita.

Alisema baada ya kupata wanaume waliowaoa wanafunzi hao kisha kuwatorosha katika kijiji hicho na kwenda kuwaficha kituo cha shule ya Ngunya Manispaa ya Morogoro, kwa lengo la kuficha ushahidi. Alisema walipelekwa katika kituo hicho ili wasome, huku wakiwa wanaendelea na majukumu mengine ya kifamilia, kwani wanaume wao waliwapangishia vyumba vyao vya kuishi.

Kutokana na hali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro alifika katika kituo hicho kilichoko Oilcom Nanenane na kuwakamata wanafunzi hao wote na kuwarudisha nyumbani kwao kwa ajili ya kijiunga na shule waliyochaguliwa.

# Waziri akuta 'maajabu' ofisi za TTCL Kibaha

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

NAIBU Waziri Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Kundo Mathew, juzi alitembelea ofisi za Shirika la Mawasiliano (TTCL) na kukuta watumishi wakifanya kazi katika ofisi chakavu huku wengine wakitumia makontena kama ofisi.

Akiwa katika ofisi hizo, aliingia katika ofisi ya meneja wa mkoa ambayo ni kontena huku akionyesha kutoridhishwa na mazingira yaliyopo hususani katika kutunza nyaraka na kutoa huduma kwa wateja.

"Hatuwezi kuwa na ofisi kama hizi. TTCL hatujajiweka katika mazingira ya ushindani, tunajivunia nini hapa? Namna hii tunajitangaza tunatoa huduma ya 4G?" Alihoji.

Katika baadhi ya ofisi za wafanyakazi ambazo ni makontena, madirisha yalionekana kuwa chakavu huku nyavu zikiwa zimechanika na samani za ndani nazo zikiwa si rafiki kuendelea kutumika.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka wabunge kupiga kelele bungeni wanapoona kitu hakiko vizuri kama ilivyo kwa ofisi hiyo, ili kifanyiwe kazi mapema badala ya kukaa kimya na wananchi kuilamu serikali.

Aliwataka wataalamu kubadilika kwa kushauri viongozi wao masuala ya miundombinu badala ya kukaa kimya na kusubiri maelekezo kutoka ngazi za juu.

"Meneja kaa na watu wako wape semina hata namna ya kujitolea tufanye kazi kwa tija. Sijaridhishwa kabisa na mazingira haya ya ofisi za shirika, tunatakiwa kubadilika," alisisitiza.

Meneja wa TTCL Mkoa wa Pwani, Jane Mwakalebela, alisema tangu amehamia katika mkoa huo, amekuta ofisi hizo zikiwa katika hali ambayo hairidhishi na uchakavu umezidi siku hadi siku.

Akiwa katika kijiji cha Kitomondo, Naibu Waziri alitembelea mnara wa Halotel na kuagiza watoaji wa huduma wahakikishe kabla hawajaweka minara wanapitia kwa mkurugenzi wa halmashauri.

Naibu Waziri alitoa agizo hilo kutokana na malalamiko ya mmiliki wa eneo uliipowekwa mnara, Rajabu Rajabu, kwamba analipwa malipo kiduchu na ardhi yake ilichukuliwa bila kuwa na maelewano mazuri.

"Mheshimiwa Waziri eneo langu hili nalipwa Sh. 50,000 kwa mwezi, lakini kabla hatujakubaliana kuhusiana na kiwango cha malipo, waliniambia nitake nisitake eneo langu wataweka mnara kwani ardhi ni mali ya serikali. Ilinilazimu kukubali kupokea kiasi hicho," alisema.

Kundo alisema kila alipopita kukagua minara, amekutana na malalamiko yanayoelekezwa Halotel huku baadhi ya maeneo wakituhumiwa kuchukua maeneo bure.

Alimtaka Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Mhandisi Martine Ntemo, kufuatilia suala la mmiliki wa ardhi hiyo apatiwe mkataba na pia kupata taarifa za kibenki ili kujua nani analipa fedha hizo.

Mbunge wa Kibaha Vijijini, Michael Mwakamo, alisema utaratibu wa kutwaa ardhi upo kisheria, lakini kuna tatizo linaloendelea kwa baadhi ya watu wanapotafuta maeneo ya kuwekeza hasa vijijini kwa kutumia njia zisizo sahihi.

HABARI KITAIFA

# Maelfu kupata ajira za kuchenjua madini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

TAKRIBAN ajira 3,000 zinatarajiwa kuzalishwa katika wilaya za Ngara na Kahama kutokana na ujenzi wa kinu cha kuchenjua madini ya Nickel kwenye mgodi wa dhahabu Buzwagi wilayani Kahama mkoani Shinyanga.

Kinu hicho kinatarajia kujengwa na Kampuni ya Tembo Nickel ya wilayani Ngara mkoani Kagera.

Hayo yalibainishwa jana na timu ya wataalamu wa serikali na mwekezaji wa kampuni hiyo waliozuru wilayani Kahama kuangalia maeneo ya kujenga mtambo wa kuchenjua madini hayo yatakayokuwa yanachimbwa wilayani Ngara mkoani Kagera.

Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Kabanga Nickel, Chris Showalter, alisema ujenzi wa kinu hicho cha kuchenjua madini utakapokamilika, zaidi ya watu 3,000 wanatarajiwa kupata ajira.

**Uwekezaji huo kwa upande wa Wilaya ya Ngara mkoani Kagera wanakochimba madini hayo, utawezesha watu 2,000 kupata ajira.**

Showalter alisema uwekezaji huo kwa upande wa Wilaya ya Ngara mkoani Kagera wanakochimba madini hayo, utawezesha watu 2,000 kupata ajira.

Kamishna wa Tume ya Madini, Profesa Abdulkarimu Mruma, aliyeongoza timu ya wataalamu wa madini kutoka wizarani, alisema serikali imetoa eneo la uwekezaji katika mgodi wa Buzwagi ili kurahisisha usafirishaji wa madini yatakayokuwa yanachenjuliwa kwenye kinu hicho.

Profesa Mruma alisema kinu hicho kinajengwa huko kutokana na kuwapo uwekezaji wa migodi mikubwa miwili ya Bulyanhulu na Buzwagi na utatumika pia kuchenjua makinikia ya dhahabu badala ya kusafirishwa kwenda nje ya nchi.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Telack, alisema serikali imeandaa maeneo manne ya ujenzi wa mitambo ya kuchenjua madini ya Nickel na kilichobaki ni mwekezaji kuchagua eneo mojawapo ambalo ataona linafaa kwa ajili ya kujengwa kiwanda hicho.

Telack alimpongeza Rais John Magufuli kwa busara yake katika kuamua ujenzi wa kinu hicho katika Wilaya ya Kahama kwa kuwa utatoa fursa za ajira kwa vijana walioko mitaani na tayari serikali imeshaandaa maeneo ya ujenzi huo yanayokidhi mahitaji katika mgodi wa Buzwagi.

Akizungumzia ujenzi wa kinu hicho, Meneja Mkuu wa Mgodi ya Bulyanhulu na Buzwagi, Benedict Busunzu, alipongeza kampuni ya Tembo Nickel kwa kuamua kujenga kinu hicho.



Mlengwa wa mpango wa kunusuru kaya maskini TASAF kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii, Njile Malambi mkazi wa kijiji cha Ipililo, wilayani Maswa mkoani Simiyu, akionyesha mifugo yake ambayo ameipata kupitia fedha za mpango huo na kumtoa kwenye umaskini. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Elimu ujasiriamali yawainua walengwa wa TASAF Simiyu

**Na Marko Maduhu,** SIMIYU

WALENGWA wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) katika Kijiji cha Ngulyati Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu, wameanzisha kikundi cha utengenezaji wa bidhaa mbalimbali za ujasiriamali na kujikwamua kiuchumi.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Ujasiriamali cha Walengwa wa TASAF katika Kijiji cha Ngulyati, Helena Amosi, alibainisha mafanikio hayo wakati maofisa wa TASAF kutoka makao makuu walipofanya ziara kuangalia maendeleo ya walengwa.

Alisema walijiunga kwenye kikundi wakiwa walengwa wanane na kuchangisha fedha ambazo wanazipata kupitia TASAF, na kuamua kutengeneza bidhaa sabuni, mafuta ya kupaka, shampoo na batiki, ambazo zimewainua kiuchumi na kuuaga umaskini.

Katibu wa kikundi hicho, Marysiana Radslausi, alisema kwa sasa maisha yao yamebadilika kiuchumi tofauti na awali, ambapo kila baada ya miezi sita huwa wanagawana faida na kwenda kuhudumia familia zao, ikiwamo kununua chakula na mahitaji ya shule.

Mratibu wa TASAF Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu, Cephline Bududi, alisema kabla ya kuwapatia fedha walengwa hao, huwa wanawapatia kwanza elimu ya ujasiriamali ili wazitumie vizuri na kuondokana na umaskini.

## Wachimbaji wadogo waomba benki ya madini

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

WACHIMBAJI wadogo wa dhahabu katika Mgodi wa Nkandi Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga wameomba Serikali kuangalia utaratibu wa kuanzisha benki ya madini itakayowasaidia kukopa na kuendesha shughuli zao za uchimbaji vizuri.

Hayo yalibainishwa juzi na katibu wa Mgodi wa Nkandi, Mdachi Shabani, alipozingumza na wanahabari waliotembelea mgodi huo kwa lengo la kuona changamoto zinawakabili wachimbaji hao.

Shabani alisema wachimbaji hao wameshindwa kuhimili kukopa fedha katika taasisi mbalimbali za ferdha kutokana na kutokuwa dhamana, hivyo kuendelea kuchimba kwa mfumo wa zamani.

Mwenyekiti wa mgodi huo, Christopha Kanjo, aliishukuru Serikali kwa kuwathamini wachimbaji wadogo kwa sasa na kusisitiza kuwa hawatamwangusha Rais John Magufuli kwani sekta hiyo imewasaidia hata kusomesha watoto wao.

## Mbunge ampongeza JPM miradi mikubwa

**Na Halfani Chusi**

MBUNGE wa Kibamba, Issa Mtemvu, amempongeza Rais John Magufuli kwa kuzindua miradi mikubwa ikiwamo Kituo cha Mabasi cha Magufuli, Daraja Kijazi na kuwapatia eneo lenye ukubwa wa hekta 75 kwa ajili ya kufanyia shughuli za kijamii.

Alitoa pongezi hizo jana alipozungumza na waandishi wa habari katika ofisi zake zilizoko Luguruni, Kibamba wilayani Ubungo.

Mbunge huyo alisema mbali na kuzindua miradi mikubwa katika Manispaa ya Ubungo, Rais alilikubali ombi lao la ardhi kwa ajili ya uwekezaji na akawapatia hekta 75.

"Mheshimiwa Rais ametupatia hekta 75 kwa ajili ya miradi ya kimaendeleo ambapo sasa katika eneo hilo, tunatarajia kuweka sehemu kwa ajili ya huduma za kijamii, sehemu ya michezo mbalimbali, jengo la wazee, soko kubwa la kumudu wingi wa watu uliopo, kutenga eneo la maziko, kuweka shule yenye kidato cha kwanza hadi sita," alifafanua.

Pia aliongeza kuwa Rais Magufuli amekuwa akitoa mchango mkubwa wa kifedha katika jimbo hilo na kwa kiasi kikubwa wamefanikisha mambo mengi kupitia huruma zake.

"Rais Magufuli alitoa zaidi ya Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali ya Wilaya Baruti, akatoa tena zaidi ya Sh. milioni 200 kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali ya Sinza Palestina.

"Pia alitoa tena Sh. milioni 400 kwa ajili ya Kituo cha Afya Kimara, akatoa Sh. bilioni tatu kwa ajili ya jengo la halmashauri. Hii inaonyesha ni kwa jinsi gani Rais wetu mtetezi wa wanyonge alivyotupigania watu wa Manispaa ya Ubungo," alisifu.

Aliwataka madiwani wote 14 walioko katika jimbo lake kuhakikisha wanafanya kazi kwa weledi na kuzingatia maslahi ya umma.

# Wataka ujenzi mabweni kunusuru vifo wanafunzi

**Na Christina Haule,** MVOMERO

WADAU mbalimbali wa elimu zikiwamo taasisi za fedha, wameombwa kusaidia ujenzi wa mabweni Shule ya Sekondari Diongoya, Turiani wilayani Mvomero, ili kuepusha vifo vya wanafunzi kutokana na kusombwa na maji.

Ombi hilo limetolewa kutokana na wanafunzi watatu kupoteza maisha kwa miaka miwili tofauti baada kusombwa na maji wakati wakivuka Mto Mbulumi kwenda shuleni.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Diongoya, Remmy Mpagama, alisema hayo juzi wakati akizungumza mbele ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Albinus Mugonya, baada ya kupokea vitu mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 18.5 kwa ajili ya shule na hospitali kutoka Benki ya NMB Kanda ya Mashariki.

**Wanafunzi wawili wa kidato cha pili walishindwa kufanya mtihani mwaka 2020 baada ya kushindwa kuvuka Mto Mbulumi ulipokuwa umejaa maji.**

Alisema katika msimu wa mvua za masika mwaka 2018, shule hiyo ilipoteza wanafunzi wawili na mwaka 2020 mwanafunzi mmoja baada ya watoto hao kusombwa na maji wakati wakivuka Mto Mbulumi ulioko karibu na kijiji cha Digalama wakati wakienda shuleni.

Pia alisema wanafunzi wawili wa kidato cha pili walishindwa kufanya mtihani mwaka 2020 baada ya kushindwa kuvuka Mto Mbulumi ulipokuwa umejaa maji.

Alisema ujenzi wa mabweni shuleni hapo utasaidia kuondoa adha wanazopata wanafunzi wanaokaa kwenye vijiji vya Digalama na Digoma wanaotembea umbali mrefu hadi kufika shuleni.

Mpagama alisema shule nyingi zenye ufaulu mzuri wilayani hapa ni zile zenye mabweni ikiwamo Shule ya Sekondari Muscat na kusisitiza kwamba wakipata mabweni watafaulisha vizuri zaidi.

Mmoja wa wanafunzi wa kidato cha nne katika shule hiyo, Shakira Mohamed, aliishukuru NMB kwa msaada wa viti na meza waliowapa. Hata hivyo, aliwaomba kuwasaidia kupata mabweni ambayo yatasaidia kuwapunguzia adha wenzao wanaotembea umbali mrefu kufika shule kwa kutumia usafiri wa baiskeli.

Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Mugonya, aliiomba NMB licha ya kuwa na moyo wa kuwachangia kila wanapopeleka maombi, kuangalia suala hilo katika mtazamo chanya huku serikali ikijipanga kutatua matatizo mbalimbali ya elimu wilayani hapa.



Wadau wa maendeleo ya Musoma Vijijini, mkoani Mara, wakiongozwa na Mbunge wao, Prof. Sospeter Muhongo (mwenye fulana ya bluu), wakikagua ujenzi wa moja ya madaraja kwenye barabara ya Musoma hadi Busekera, eneo la Kijiji cha Kusenyi juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri ataka kasi miradi ya bandari

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leonard Chamriho, ameigiza Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), kuhakikisha miradi ya uboreshaji wa gati na miradi mbalimbali katika Bandari ya Dar es Salaam inakamilika kwa wakati.

Dk. Chamriho aliotoa maagizo hayo jijini Dar es Salaam alipofanya ziara ya kutembelea miradi inayoendelea katika bandari hiyo na kukabidhiwa gati namba tano.

Alisema Bandari hiyo ya Dar es Salaam ndio kitovu kikuu cha ukusanyaji wa mapato na ndio maana serikali imeweka nguvu yake kubwa kuhakikisha inaboreshwa zaidi ili kukusanya mapato zaidi ya yale yanayokusanywa sasa.

Alisema jumla ya magati nane yanaboreshwa katika bandari hiyo ya Dar es Salaam, na kwamba kati ya hayo manne yamekamilika na yameanza kutumika.

Alisema kukamilika kwa magati yote yatachagiza kasi ya ukusanyaji wa mapato kwa kiwango cha juu zaidi.

"Julai mosi mwaka 2017, Rais John Magufuli aliweka jiwe la msingi la mradi huu wa uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam kwa awamu ya kwanza, kwa kuboresha magati nane, saba ya zamani na moja mpya," alisema Dk. Chamriho.

"Na katika maboresho hayo, gati namba sifuri, namba moja mpaka nne yamekamilika na yameanza kutumia, niwapongeze sana TPA kwa kufanikisha usimamizi huu japokuwa changamoto ni kwamba mradi huu unafanyika huku huduma ikiendelea."

Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Deusdedit Kakoko, alisema kusudio lao ni kuhakikisha mpaka kufikia mwaka 2025 wanafikisha shehena tani 25 kwa mwaka kutoka za tani milioni 17.5 za Juni mwaka jana.

## Sababu Tarime kukwama kununua gari la mil. 200/-

**Na Samson Chacha,** TARIME

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Tarime Mjini limepinga ununuzi wa gari la halmashauri lenye thamani ya Sh. milioni 200, kutokana na ufinyu wa bajeti.

Madiwani walipitisha bajeti ya Sh. bilioni 30.2, huku fedha za kununulia gari hilo zielekezwe kwenye miradi ya maendeleo.

Akizungumza katika kikao cha baraza la madiwani lililokuwa linapitisha bajeti yake chini ya Mwenyekiti wake Daniel Komote na Mkurugenzi wake, Elias Ntirihungwa , Mbunge wa Tarime Mjini, Michael Kembaki, alisema baraza limepitisha bajeti ya mwaka 2021/2022 ya Sh. bilioni 30.2, na kwamba wamebadili mpango wa ununuzi wa gari la Halmashauri kwa Sh. milioni 200 badala yake fedha hizo zitaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa madarasa , nyumba za walimu , vituo vya afya , zahanati, barabara na maji.

Mkurugenzi Ntirihungwa, alisema kuwa bajeti ya mwaka huu 2021 /2022 ya Sh. bilioni 30.2 imezidi ya mwaka 2020/2021 ya Sh. bilioni 19.7.

## Mashirika yatoa elimu mazingira

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

TAASISI ya Kuendeleza Nishati Asili Tanzania (TaTeDo) kwa kushirikiana na Shirika la WWF wameanza kutoa mafunzo kwa wajasiliamali wadogo wanawake zaidi ya 20 kutoka katika vikundi 10 wilayani Masasi mkoani Mtwara kuhusu mazingira.

Mafunzo hayo ni ya kuwajengea uwezo wa umuhimu wa matumizi bora ya nishati isiyotokana na miti na kupunguza matumizi ya kuni na mkaa, nishati ambazo zinachangia katika uharibifu wa mazingira ikiwamo misitu.

Aidha,wajasiliamali hao pia wamefundishwa jinsi ya kutumia majiko sanifu na utengenezaji bidha za vyakula ikiwamo keki, skonzi na mikate kwa kutumia mkaa na kuni kwa kiasi kidogo.

Mafunzo hayo ya siku tatu yalifanyika wilayani Masasi mkoani hapa na kusimamiwa na Halmashauri mbili zilizopo wilayani Masasi ambazo ni Halmashauri ya Mji Masasi na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi.

Mratibu wa mafunzo kutoka TaTeDo, Elizabeth Sorwa, alisema mpango huo wa utoaji mafunzo utaendelea kutekelezwa ili kupunguza athari za uharibu wa mazingira.

Sorwa alisema mashirika hayo mawili yapo kwa ajili ya kusimamia na kulinda mazingira na miradi mikubwa inayokuwa ikiifanya inajikita zaidi katika kupunguza matumizi ya mkaa na kuni.

ama
ALHAMISI MACHI 4, 2021
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Mambo sita yaliyosaidia corona ipunguze makali barani Afrika**



**Wakulima wanavyohamishiwa katika sayansi upimaji udongo kabla ya jembe**

Ukurasa 13



Ukurasa 14

**Pata sababu kuu za janga la gesi kujaa tumboni na madhara yake**

## SAMIA SULUHU HASSAN:

# Msifungie watoto wenye matatizo, waibueni wakatibiwe, haki zao zipo

## •Waziri Afya: Sera yao shirikishi inakuja

**Na Yasmine Protace**

MAGONJWA adimu yana historia ya kusababisha baadhi ya wazazi kuwaficha majumbani watoto wao, huku kukiwapo historia mbaya ya baadhi yao hawapelekwi masomoni.

Inaelezwa kwamba, hata kama mtoto anaugua magonjwa adimu, anayo haki ya kutofichwa na kupelekwa hospitalini kujua namna ya kumsaidia.

Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, anasema kuna baadhi ya watu wanapojifungua na kupata watoto, wanajikuta kuangukia matatizo ya magonjwa ya kudumu, wenguine kuwa na uthubutu mbaya wa kuwatelekeza.

Pia, anasema wapo kinamama wanaangukia kutengwa na waume zao, pindi tu inapobainika mtoto wao anasumbuliwa na magonjwa adimu, yanayoendana na baadhi ya wazazi kushindwa kuwapeleka masomoni.

Ujumla wa hali hiyo unachangia kumnyima haki mtoto asipate elimu. Mtazamo mkuu ni kwamba, haja ya kuwapo busara magonjwa adimu hayapaswi kutumiwa na wazazi kuwa kigezo cha kuwanyima haki watoto, pale wanapokuwa na magonjwa.



Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan, alipohutubia Maadhimisho ya Siku ya Magonjwa Adimu Duniani yaliyoadhimishwa Februari 28, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO.**

Makamu wa Rais Samia, anasema serikali imejiandaa kuhakikisha watoto wenye magonjwa, wanapata haki sawa na hawaachwi nyuma katika kuwapatia huduma za msingi za aina zote.

Ni mtazamo anaouwakilisha katika Maadhimisho ya Siku ya Magonjwa Adimu Duniani, yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, ambao umezaa wajibu wa wazazi kuhakikisha makundi yote ya kijamii yananufaika ndani ya harakati za kushughulikia magonjwa adimu.

Pia, anasema ni haki na kawaida ya watoto walio na magonjwa adimu, wanaangukia mpambano sawa na wasio na magonjwa ya kundi hilo, kupata tiba na unafuu wa afya.

"Serikali haijawaacha nyuma watoto hao na Ina nia dhamira na sababu ya kufanya mazingira wezeshi ya kuwahudumia kwani magonjwa hayo ni kama magonjwa mengine," anasema.

Wito wake wa jumla, ni kwamba wazazi wenye watoto wa hali hiyo waongeze sauti za kuweza kuwaamsha wengine waajitokeze, hali itakayoisaidia serikali kubaini haja iliyopo ya kutoa matibabu sawa.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, katika hilo ameahidi Wizara yake ipo tayari kupokea maoni na mawazo kutoka kwa wadau na wazazi wenye uzoefu wa kuwahudumia watoto wenye magonjwa adimu.

Anasema mapitio ya sera hiyo mpya, iwe na sura inayotambua na mapambano yanayotakiwa kufanywa kwenye eneo hilo na hadi sasa wizara yake itaendelea kushirikiana na wadau, pamoja kutengeneza mpango mkakati wa kukabiliana na magonjwa hayo.

AFYA

# Mambo sita yaliyosaidia corona ipunguze makali barani Afrika

## • Mikakati inayotajwa nchini imo • Nafasi ya darasa la janga ebola

**Na Maulid Mmbaga**

NCHI nyingi za Afrika zinasifiwa duniani kudhibiti kusambaa virusi vya corona, licha ya mifumo ya afya katika baadhi yake kutoridhisha.

Takwimu zilizokusanywa na Chuo Kikuu cha John Hopkins, Marekani zinasema Afrika yenye wakazi zaidi ya bilioni moja (makadirio ya mwaka jana bilioni 1.3), hadi sasa kuna zaidi ya wagonjwa milioni 1.5 waliothibitishwa na virusi vya corona.

Ripoti yake ya utafiti wa ubia na mashirika kadhaa binafsi kubaini corona inavyoshughulikiwa Afrika, inaonyesha athari ndogo kwa Waafrika, kulinganisha na kwingineko duniani.

Mkuu wa Afrika wa Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (Africa CDC) Dk, John Nkengasong, alishatamka kwamba viwango vya chini vya upimaji watu katika baadhi ya nchi unaendelea kuwa kikwazo cha kukabiliana na ugonjwa huo.

Yafuatayo ni mambo yanayoifanya Afrika kuwa na kasi ndogo kukabili corona, kulinganisha na kwingineko duniani:



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alipotembelea ofisi za Taasisi ya Tafiti na Uchunguzi wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) iliyopo Mabibo, Dar es Salaam na kukagua ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza dawa za binadamu, kwa kutumia miti dawa asilia, kukabili magonjwa ya mlipuko. **PICHA: MTANDAO.**

### JOTO KUBWA

Mtafiti Mkuu wa Chuo Kikuu cha Maryland, Marekani Mohammad Sajadi, anasema kumebainika uhusiano kati ya hali ya hewa na kusambaa maambukizi ya corona. IMAGES

"Tulichunguza mambo ya awali ya virusi katika miji 50 duniani na tulibaini virusi vilisambaa kwa urahisi katika maeneo yaliyokuwa na viwango vya chini vya joto," anasema, ingawa anakiri penye dalili ya baridi panaendana na kasi ya virusi kusambaa.

Nchini Afrika Kusini kunakokadiriwa kuwapo nusu ya maambukizi na vifo ya corona barani Afrika, kuligundulika maambukizi kuongezeka msimu wa baridi, tofauti na mikasa ya msimu wa joto.

### KUNA VIJANA WENGI

Umoja wa Mataifa unafafanua nchi za Afrika zina vijana wengi, kuliko wazee, ikitajwa kuchangia kasi ndogo ya maambukizi.

Shirika la Afya Duniani (WHO), linataja vifo vingi kutokana na corona, wengi wanakadiriwa kuwa na miaka zaidi ya 80, wakati Afrika ina vijana wengi wenye umri chini ya miaka 19.

"Janga hilo halijaathiri watu walio na umri mdogo. Karibu asilimia 91 ya maambukizi ya virusi katika eneo la Kusini mwa Jangwa la Corona ilikuwa ni ya watu walio chini ya miaka 60 na zaidi ya asilimia 80 ni ya wale ambao hawaonyeshi dalili," inafafanua WHO.

Mkuu wa WHO Ukanda wa Afrika, Dk. Matshidiso Moeti, anasema ni eneo lenye asilimia tatu ya watu wanaozidi miaka 65, ikilinganishwa na Ulaya, Amerika Kaskazini na nchi tajiri barani Asia, wanakopatikana wazee wengi.

"Moja ya sababu iliyochangia idadi kubwa ya maambukizo ya virusi vya corona katika nchi za Magharibi, ni kwamba wazee walikuwa wanaishi katika makazi maalumu na suala hilo lilisababisha virusi kusambaa kwa kasi," anaeleza.

Dk. Matshidiso anasema, wazee wengi Afrika wamejitenga vijijini na ngumu kuwafikia, wachache ndio wanapatikana mijini, hali inayotokana na utamaduni wa watu wengi Afrika kurudi vijijini walikotoka wanapostaafu kazi.

### DAWA ASILI ZINATENDA

Afrika inasifika kwa utajiri wa dawa za asili na wataalamu wengi wanaotibu magonjwa, hata ya milipuko kama corona.

Nchini Tanzania, pamoja na tahadhari za kisayansi zinazoendelea, tiba asili zinapewa kipaumbele, ikiwamo kujifukiza na kutumia dawa za asili zilizothibitishwa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR).

Kuna dawa za asili kadhaa zilizokwishaidhinishwa kutibu homa ya mafua na matatizo ya mfumo wa upumuaji, sasa ni kimbilio la wananchi.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Dk. Dorothy Gwajima, anasema serikali kwa kutambua umuhimu wa tiba asili, imefikia hatua ya kujenga kiwanda cha kuchakata dawa asilia chini ya NIMR.

Hadi sasa katika jitihada za kukabili magonjwa ya mlipuko kitaifa, kuna ujenzi unaoendelea eneo la Mabibo, jijini Dar es Salaam.

### MIFUMO BORA WA AFYA

Janga la corona lilikuja, wakati Jamhuri ya Kidemokrasia Congo (DRC), inapambana na mlipuko wa ugonjwa ebola na nchi jirani ziliwekea mikakati wa kujikinga na maambukizi, kwa kufanya uchunguzi wa afya za wasafiri wanaoshukiwa na ebola, hali iliyorahisisha vita katika mlipuko wa ebola.

Nchi kadhaa za Afrika Magharibi zilikabiliana na ebola, kati ya mwaka 2013 na 2016, hali iliyosaidia uelewa kukabili corona, hapo ikijumuisha mbinu ya kuwatenga washukiwa au waliothibitika kuambukizwa.

Nchini Nigeria, wahudumu afya walizunguka vijijini kuwapa watoto chanjo za polio, wakichukua wakichukua nafasi kuelimisha jamii kuhusu corona.

Aidha, licha miundombinu duni ilyopo Afrika, nguvu yake nyingi iko katika mifumo ya afya jamii inayowasaidia kukabili changamoto zilizopo.

### HATUA ZA HARAKA

Mkasa wa kwanza wa maambukizi ya corona, ulitajwa kutokea nchini Misri Februari 14 mwaka jana. Mataifa yaliyoendelea, yalitabiri huenda virusi vingewawaathiri vibaya Waafrika, kutokana na mifumo duni ya kiafya kwa nchi zake.

Hata hivyo, utabiri uligonga mwamba baada ya nchi za Kiafrika zilipochukua hatua za dharura kudhibiti ueneaji virusi kwa mafanikio kiasi fulani.

Miongozo ya afya ya umma; kutosalimiana kwa kugusana mikono; kunawa mikono kila mara; kutokaribiana; na kujihami kwa kuuvaa barakoa, umezingatiwa.

Nchini Lesotho yenye raia zaidi ya milioni mbili, kulichukuliwa hatua ya uzuiaji kabla ya kuwapo maambukizi ya corona na ilitangaza dharura, ikafunga shule zote Machi, mwaka jana.

Mengine yalihusu amri ya kutotoka nje kwa zaidi ya wiki tatu, ikiwa ni hatua ya kushirikiana na nchi zingine Afrika na ilipofioka Mei, mwaka huo, amri ya kutotoka nje iliondolewa, pale Lesotho ilipomtangaza mgonjwa wa kwanza.

### UMMA UNATOA MSAADA

Ripoti ya utafiti iliyofanywa na asasi ya PERC katika nchi 18 mwezi Agosti mwaka jana, unatamka nafasi ya msaada wa umma na ikagundulika wastani wa asilimia 85 ya wakazi walikuwa wavaaji barakoa.

"Kutokana na utekelezaji wa muongozo wa afya ya umma na msaada wa kijamii, nchi wanachama wa muungano wa Afrika zilifanikiwa kudhibiti virusi vya corona kati ya mwezi Machi na Mei 2020," inasema PERC.

Ripoti hiyo inafafanua kwamba kulegezwa masharti katika miezi kati ya Juni na Julai 2020, kulisababisha ongezeko la maambukizi ya virusi vilivyoripotiwa katika nchi tofauti za Afrika.

Baada ya wakati huo tena, maambukizi na idadi ya vifo vimeonekana kushuka Afrika, huku hali ya awali ilihusishwa na msimu wa baridi kali.

Utekelezaji masharti ya kudhibiti maambukizi, unatajwa kuendana na changamoto kama mashirika mengi kufungwa na kupoteza umma ajira kwa kiwango kikubwa. Kunatajwa kupotezwa ajira milioni 2.2 nchini Afrika Kusini, katika nusu ya kwanza ya mwaka jana.

Baadhi ya nchi ziliruhusu biashara kuendelea, licha ya kuripotiwa maambukizi mengi. Watafiti wa PERC, wanasema uamuzi huo ni zao la maoni ya umma, kukiwapo wastani wa watu sita kati ya 10 walitaka uchumi ufunguliwe, kwani jambo muhimu zaidi ni kuzingatiwa mwongozo wa afya.

MAZINGIRA

# Wakulima wanavyohamishiwa katika sayansi upimaji udongo kabla ya jembe

## •Wenyewe waamka nayo 'kumbe hivi!'

**Na Woinde Shizza, ARUSHA**

NI kitu ambacho mtu amekizoea. Ni tabaka la juu ya ardhi ambako mimea inaota na kuna mchanganyiko wa vipande vidogo vya mwamba na madini yaliyosagwa, mabaki ya mimea na wanyama yaliyooza (mboji).

Hali kadhalika, ni mazingira yanayojumuisha uwapo wa wadudu wa aina tofauti, pia hewa na maji yanayojaza nafasi katikati ya vipande vidogo vya mwamba.

Udongo wenye afya ni msingi muhimu katika kilimo. Rutuba ya shamba hupungua kadri kunavyopandwa na kuvunwa mazao, jambo linalojenga mantiki ya umuhimu kufahamu afya ya udongo shambani, kujenga upeo wa kutunza rutuba ya kilimo endelevu, mbegu bora, mbolea.

Inaelezwa kwamba, kila mmea unapomea huhitaji virutubisho katika ukuaji na inafika wakati virutubisho hivyo hupungua au kwisha katika udongo, hali inayopunguza rutuba ya shamba.

Inafafanuliwa kitaalamu kwamba, pindi rutuba ya udongo inapoisha au kupungua, inachangia wakulima wengi kuhamia sehemu nyingine wanaodhani kuna rutuba wakianzisha mashamba mapya, hali inayochangia katika uharibifu wa mazingira.

Kufahamu udongo ndio unafungua elimu ya virutubisho vilivyopo shambani na kumsaidia mtu kujua aina ya mbolea inayomfaa shambani, kiasi chake, wakati wa kuweka mbolea na kuongeza uzalishaji, hali inayosaidia kupunguza gharama.




Shamba darasa kwa la ardhi ambayo udongo wake umepimwa, wilayani Arumeru.

### UELEWA WA WAKULIMA

Uchunguzi wa Nipashe, umethibitishiwa upungufu wa wakulima wengi kukosa elimu ya upimaji udongo na wapo wasiojua hata kuwapo msamiati 'kupima udongo.'

Mwandishi wa gazeri hilo alipozungumza na mkulima kutoka kijiji cha Likamba, wilayani Arumeru, mkoa wa Arusha, anaeleza uelewa wake kuhusu udongo, ni kwamba unausaidia mmea kukua kwa kushirikiana na maji, lakini hajui umuhimu wa virutubisho vyake.

"Mimi napanda shamba langu kawaida tu, sijui kuhusu suala la afya ya udongo kuna wakati napata mazao ambayo naona ni kawaida na kuna wakati sipati kabisa na hilo nalichukulia kuwa linatokana na msimu na wakati mwingine tunaambiwa kuwa shamba limechoka kulimwa zao moja kila mwaka," anasema Winifrida.

Neema Wilson, mkazi wa kijiji hicho naye anaungana na uelewa huo, kwamba hajui kama umuhimu tofauti wa udongo, huku kilimo chake ni kwa ajili ya chakula, huwa anauza pindi anapokumbwa na magumu ya maisha.

Anasema, katika shamba lake la ekari mbili, kila mwaka idadi ya mavuno yanatofautiana na alikuwa anaelewa kuwa ni zao la mvua kwa kipindi hicho na hakujua mchango wa udongo na hali ya hapo.

Mkulima Lomayani Lotha, anachangia akisema binafsi hajawahi kusikia kinachohusiana na upimaji udongo na alichokizoea ni kilimo cha kawaida pekee, alichoshuhudia na kukiendesha tangu zama zilizopita.

Sasa ana mtazamo mpya, waelimishwa zaidi kuhusiana na kilimo hicho, ili nao walime kilimo cha uhakika kinachopatia mazao mengi yenye ubora na tija.

Anthony Mosha, mkulima aliyepata darasa la uelewa kuhusu upimaji afya ya udongo kutoka maeneo ya Njombe na Lupembe, anaeleza namna tangu alipopima udongo shambani, umempatia manufaa katika kilimo cha maparachichi na mahindi yanayotoa mazao mengi.

Mosha anasema, baada ya kufanya vipimo majibu yalionyesha kwamba hakuna udongo mzuri na akaelekezwa, namna ya kuurutubisha na hatimaye akafanikiwa.

"Kabla ya kuja, mazao yalikuwa 'yanaita', lakini yanadumaa, ila hivi sasa tunapoongea maparachichi yanarefuka na hata nikipanda mahindi yanakuwa mazuri na napata mazao mengi," anasema mkulima Mosha.

Fabian Mwambinga, anayelima maharage ndani ya Halmashauri ya Arumeru, anasema awali alipoanza alipata hasara kubwa hadi ikamkatisha tamaa ya kuendelea na kilimo.

Anasema, alilima maharage katika shamba la ekari tatu na kupata magunia matatu. Anaendeleza simulizi: "Nilidhani nikiweka mbolea ndio nitapata mazao mengi, lakini nilipokuwa nikienda kununua mbolea ndipo nilipokutana na kampuni hii ya kupima afya ya udongo.

"Walinishauri nipime udongo kwanza kabla ya kulima, ndipo wakanipimia na kukuta udongo wangu hauna tatizo la rutuba, bali lina tatizo la 'pH' (chumvi chumvi na tindikali) na kunieleza niweke chokaa ya kilimo.

"Na baada ya kuweka nilipotesha katika shamba lile lile nilipovuna awali nikapata gunia tatu nilipovuna baada ya kuweka chokaa katika shamba lilelile la ekari tatu nilipata gunia 18."

Hadi sasa kuna ushauri kwamba kupima uhalisia wa udongo inakuwa gharama ndogo kwao wakulima, ikiilinganishwa na gharama za kulima.

### MTAALAMU UDONGO

Mkurugenzi wa kampuni binafsi inayojishughulisha na upimaji udongo kwa wakulima wakubwa, wakati na wadogo (LSSL) Dk. Edmond Matafu, anasema elimu ya umuhimu wa afya ya udongo ambayo bado haijafikiwa na wakulima wengi, inawafanya waendelee kufanya kilimo cha mazoea.

Hivyo, ni muhimu kwa wakulima kupata elimu ya umuhimu wa kupima afya ya udongo, ili walime kwa tija kwao na taifa kwa ujumla.

Dk. Matafu anasema, hadi sasa kuna faida kubwa za kupima udongo moja wapo ikiwa kujua aina ya mazao yanayofaa katika shamba la mkulima, kujua virutubishi vya udongo na kiasi cha mkulima anapaswa kununua, kulingana na upungufu wa virutubishi vinavyohitajika.

"Hii itasaidia kupunguza gharama, kwani wakulima wamekuwa wakitumia mbolea hata kwa mashamba ambayo yana virutubisho vya kutosha na wakati mwingine kutumia mbolea isiyofaa kwa eneo husika, jambo linaloongeza hasara," anasema Dk. Matafu.

Anataja umuhimu wa kusaidia utunzaji mazingira kubaini kasoro katika virutubishi vinapozidi kwenye udongo hata kuharibu mazingira ya uotaji mimea, jambo ambalo mkulima anapolima udongo shambani, inamwezesha kujua hitaji la mbolea au virutubishi vya kuuboresha udongo.

Dk. Matafu anaeleza kuhamasisha upimaji udongo, kunalenga kuwasaidia wakulima wote kujua afya ya udongo na hasa tindikali, ili kujua virutubishi vilivyomo katika udongo kabla ya kuanzisha kilimo na kuwezesha kujua kiasi cha mbolea kinacho-

Endelea Uk. 14



Wakulima wakipewa darasa la sayansi udongo na upimaji wake. **PICHA ZOTE:WOINDE SHIZZA.**

AFYA

# Pata sababu kuu za janga la gesi kujaa tumboni na madhara yake

## • Hivi hapa vyakula visababishi
## • Imo sigara; madhara ni tishio

Na Christina Mwakangale



KIAFYA kunatajwa kiwango cha kutoa gesi tumboni kwa njia yeyote, katika mwili wa binadamu ni hali ya kawaida.

Kinatajwa kiwango hicho cha kutoa gesi mwilini kuwa ni kisichozidi mara 15 kwa siku.

Inapotokea kuzidi, kitaalamu inatajwa kuwa tatizo kwa mtu wa aina hiyo, kutokana na kuzalisha gesi nyingi mwilini na anahitaji kufanyiwa uchunguzi ikiwamo vipimo na hatimaye tiba.

Daktari wa bingwa tiba za binadamu, Isaac Maro, anaeleza namna ongezeko la watu walio na tatizo la gesi hivi sasa, akitaja visababishi, athari na njia za kukabiliana na hilo.

"Kuna matatizo mengi ya gesi, watu wanachukulia kirahisi, watu wengi wana changamoto ya gesi. Kama kuna maswali mengi ambayo naulizwa ni kuhusu gesi.Mwingine anasema dokta ninywe 'magnesium'," anasema Dk. Maro.

Anasema mwili wa binadamu huingiza hewa au gesi tumboni, kwa njia mbalimbali, ikiwa ni pamoja na wakati wa mlo, kunywa maji na hata kipindi ambacho mmeng'enyo unafanyika.

"Wakati wa mchakato wa mmeng'enyo wa chakula, kuna virutubisho vingine vinaingia na kutoka. Kawaida tumboni kuna viumbe vinaishi kazi yao ni kisaidia mmeng'enyo, lakini vinahitaji kuishi," anabainisha Dk. Maro.

Anaendelea: "Viumbe hivi navyo vinakula na vinatoa gesi na kisha mtu anatoa gesi, kuna sababu nyingi gesi kuzalishwa tumboni.".

### GESI INAVYOHAMIA TUMBONI

Dk. Maro anasema chanzo cha tatizo la gesi mwilini, ambayo kwa kiasi kikubwa inaanza tumboni hasa wakati wa kula, hewa inaingia kwa wingi.

Mtaalamu huyo anataja sababu ya pili, ni wakati wa kunywa maji hewa nyingi huingia tumboni, pamoja na ulaji vichangamsha kinywa kama vile bazooka.

Kwa mujibu wa mtaaluma huyo, utumiaji vinywaji vya sukari villivyo na gesi au vilivyosindikwa kutoka viwandani ni sababu ya tatu gesi kuwa nyingi tumboni.

Dk. Maro anaorodhesha sababu ya nne, ambayo ni ulaji chakula kwa haraka haraka pasipo a kupumzika, nayo inagaukia katika kusababisha gesi nyingi tumboni.

"Kuna wakati hutokea kasi ya kutoa gesi ni ndogo kuliko kiwango cha hewa au gesi ambacho kimeingia mwilini na kulingana na aina ya chakula ulichokula," anaeleza Dk. Maro na kuongeza:

"Mfano mlo wa mbaazi, kunde na maharage huzalisha kiwango kikubwa cha gesi, na kusumbua tumbo."

Pia, anabainisha sababu ya tano ni kitendo cha kuchelewa kula, bila kufuata kaninu maalumu, inazalisha uwapo wa gesi tumboni.

Katika mtazanmo huyo Dk. Maro anakumbusha kwamba. ulaji wa chakula unapaswa kuwa na ratiba nzuri kulingana na muda ambao mtu anakuwa amejipangia mtu, au kufuata kanuni iliyozoeleka ya milo mitatu, asubuhi, mchana na jioni.

### MADHARA YAKE MAKUU

Dk. Maro anabainisha madhara yatokanayo na kiwango cha gesi kikubwa mwilini kwa husababisha kuzalishwa kwa tindikali kwenye kifua.

"Gesi ikizidi unakuwa unajisikia kiungulia baada ya 'acid'(tindikali) kupanda juu," anasema na kwamba kuna watu ambao gesi inapowazidia, huwasababishia kushindwa kufanya majukumu yao ipasavyo.

Hapo, ndipo inazaua madhara kama mzunguko wa damu kuharibika na kuwa mdogo, ama mgongo au kiuno kuuma, miguu, au mikono kufa ganzi, mwili kuchoka kila mara ana mhusika anakosa hamu ya kula.

"Kama unahisi unapata sana gesi nenda hospitali upatiwe dawa lakini uchunguzi kwanza, kwa sababu gesi huambatana na tindikali na kuongeza presha ndani ya tumbo kati ya mrija wa kuingiza chakula na kifuani. Presha ikizidi, mirija hii haifungi," anasema Dk. Maro.

### VYAKULA VISABABISHI HIVI HAPA

Mtalamu huyo anataja vyakula vinavyobabisha gesi tumboni, mojawapo ni mtindo wa maisha ya ambao hivi sasa watu hususan waishio mijini hula vyakula vilivyoandaliwa haraka, hasa vya kukaanga kwa mafuta.

Matumizi ya vyakula hivyo ni pamoja na vinywaji, vyakula vyenye mafuta mengi, kama vile chipsi, rosti na vilivyokobolewa kama ulaji ugali wa sembe, maandazi, chapati.

Pia, vinywaji vyenye vimelea kama kafeni nyingi, kama vile pombe, kahawa, soda na ulaji chokoleti, uvutaji sigara vyote vinasababisha chakula kutosagwa au kumeng'enywa ipasavyo tumboni kirahisi.

Wataalamu wa afya wanasema matumizi ya dawa ya vidonge vya antibaiotiki au vinavyopunguza maumivu mwilini, bila kufuata ushauri wa daktari, nayo inaweza kuwa sababu ya gesi nyingi tumboni.

Pia, kuna tatizo linalosabaishwa kwa ambao wanaougua vidonda vya tumbo au kupungua mtiririko wa damu kwenye utumbo mwembamba.

# Wakulima wahamia upimaji udongo

Inatoka Uk. 13

hitajika katika mmea.

"Kwa kupima udongo, mkulima atajua virutubishi vilivyoko kwenye udongo," anaeleza, umuhimu wa wakulima kabla ya kilimo wanapaswa kujua namna afya ya udongo shambani kwake, kuwa na kilimo chenye tija.

### UPIMAJI UNAVYOFANYIKA

Kinachofanyika ni kwa kuchukua sampuli ya udongo kwa njia ya kupishanisha (zigzag) na kupeleka katika maabara ili kujua aina ya mbolea na mazao yanayokubali katika eneo hilo.

"Majibu mazuri ya udongo yanatokana na umakini wa uchukuaji wa sampuli katika shamba ambapo anayechukua udongo anatakiwa kuchimba shimo zaidi ya 15 lenye kina kati ya sentimeta 15 hadi 20 na kukusanya sampuli hizo toka maeneo mbalimbali ya shamba analotarajia kulima," anafafanua.

Anasema baada ya kukamilika ukusanyaji wa sampuli, udongo unapelekwa katika maabara ambako majibu yanatoka ikipita siku kadhaa, ingawaje pia kuna kifaa cha kupima udongo papo kwa hapo.

"Tuna aina mbili za teknolojia za kupima udongo moja ya papo kwa hapo na nyingine ni ya maabara. Hii ndio inayotoa matokeo kwa kina zaidi, ikiwa ni pamoja na aina ya mazao yanayofaa katika shamba.

"Lakini, kuna maeneo mengine majibu yanatoka kuwa hapafai kulima zao lolote na hapa panahitajika jitihada za kurutubisha udongo," anasema.

### DALILI ZA MADHARA

Mtaalamu huyo anasema, kuna madhara mtu anapoweka mbolea pasipohitajika, mojawapo ni kuharibika au kupunguza uzalishaji wa mazao na upimaji unafanyika kuwasaidia wakulima kuongeza tija ya kilimo

DK. Matafu anasema, kuanzisha kwa huduma za upimaji udongo kumsaidia mkulima alime kilimo cha uhakika na chenye tija, pamoja na kumshauri zao ambalo linaweza kustawi katika ardhi anayotaka kutumia kwa ajili ya kilimo.



## HABARI DODOMA

# Makanisa CPCT yatangaza maombi siku 21

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BARAZA la Makanisa ya Kipentekoste Tanzania (CPCT), limetangaza siku 21 za maombi ya kufunga kwa ajili ya mambo mbalimbali ikiwamo ugonjwa wa corona.

Akitoa tamko la baraza hilo jana, Mwenyekiti wa CPCT taifa, Askofu Peter Konki, alisema hatua hiyo imetokana na kikao cha Baraza la Maaskofu kilichofanyika Februari 25, mwaka huu cha kujadili majanga yanayolikabili taifa.

Alisema maombi hayo yataanza Machi 6 hadi 26, mwaka huu nchini.

"Natoa wito kwa wanachama wa CPCT na wasio wanachama wa CPCT wanaopenda kuungana nasi katika maombi haya 21 kwa utaratibu huu ambapo kila siku saa 10 hadi 12 jioni tutakutana kuomba kanisani na tunaomba maaskofu wasimamie hili kwa uaminifu," alisema.

Alisema siku ya 21 maaskofu wakuu watakusanyika Dodoma ili kuhitimisha maombi hayo.

"Tumemuomba Rais wetu John Magufuli ikiwa ataona kibali kwake na kama ana nafasi ya kuhudhuria na kuhitimisha maombi hayo, tayari tumepeleka barua yetu, na tutahitimishia ukumbi wa Jakaya Kikwete Convention center kuanzia saa tano asubuhi hadi 12 jioni, "alisema.

Alitoa wito kwa Watanzania, viongozi mbalimbali kuungana kwenye maombi hayo na wiki ya kwanza itakuwa kwa ajili ya toba kwa kanisa na taifa.

"Wiki ya pili ni kuomba uponyaji kwa taifa dhidi ya corona, ugonjwa wa sukari, saratani, tezi dume, figo na shinikizo la damu, roho ya hofu, njaa na umaskini," alisema.

Alisema wiki ya tatu ya maombi itakuwa ni kushukuru kwamba Mungu amesikia maombi na kuponya taifa.

# Jafo amwagiza mkandarasi kukamilisha mkataba Julai

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, ameonyesha kutoridhishwa na kasi ya ujenzi wa barabara za Mji wa Serikali Mtumba na kumwagiza mkandarasi kukamilisha kwa matakwa ya mkataba wake Julai 30, mwaka huu.

Barabara hizo zenye urefu wa kilomita 52 zinajengwa kwa kiwango cha lami na mkandarasi kutoka Kampuni ya Chico.

Akikagua ujenzi huo jana, Waziri Jafo alimtaka mkandarasi kuacha visingizio na kukamilisha ujenzi huo kwa wakati.

"Mnasema ujenzi unasuasua kwasababu ya upatikanaji wa saruji aina ya 32.5N kuwa tatizo kwanini msitumie 42.5N? Mimi nashauri saruji aina ya 42.5N ifanyiwe vipimo maabara kuangalia namna itakavyopunguzwa ili itumike kumalizia barabara hizo kwa wakati na kwa ubora," alisema na kuongeza kuwa kasi ipo chini kwa asilimia sita.

**Haiwezekani mradi kuchelewa wakati kuna saruji ambayo vitu vikipunguzwa inaweza kutumika katika eneo la ukubwa huo wa saruji inayohitajika.**

"Sihitaji mjadala wa aina yoyote nataka ifikapo Julai 30, ukamilike, haiwezekani uchelewe kwa kigezo cha kukosekana saruji aina ya 32.5N hivyo angalieni namna ya kutafuta hili," alisema Jafo.

"Haiwezekani mradi kuchelewa wakati kuna saruji ambayo vitu vikipunguzwa inaweza kutumika katika eneo la ukubwa huo wa saruji inayohitajika."

Awali, akitoa taarifa kuhusu maendeleo ya mradi, Mkurugenzi wa barabara mjini, Mhandisi Mohammed Mkwata, alisema hadi kufikia mwishoni mwa Februari mwaka huu, utekelezaji umefikia asilimia 63 na ilitakiwa kuwa asilimia 69 kwa mujibu wa mpango wa kazi wa mkandarasi.

"Kuna pengo la asilimia sita dhidi ya mpango na sababu zilizochangia kuwepo kwake ni uhaba wa saruji katika kipindi cha kuanzia Novemba 26 mwaka 2020 hadi Februari 2021 ambapo tuliomba usaidizi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu katika kukabiliana na tatizo hili," alisema.

Alisema kukosekana kwa saruji aina zote 32.5N na 42.5N kwa kadiri ya mahitaji halisi iliathiri kazi za ujenzi wa vivuko na ujenzi wa tabaka la kwanza la barabara ambalo nalo linahitaji saruji.

Alisema Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kupitia Mhandisi mshauri itaendelea kusimamia mradi huo kwa karibu zaidi ikiwa ni pamoja na mkandarasi kufanya kazi usiku na mchana ili mradi ukamilike kwa muda.

"Hadi mwezi Januari mwaka huu mkandarasi amekwishalipwa kiasi cha Sh. bilioni 17, malipo yaliyo kwenye mchakato wa malipo ni Sh. bilioni 8.8, mhandisi mashauri amewasilisha hati za madai zenye jumla ya Sh. milioni 446 na bado hajalipwa," alisema.

Katika hatua nyingine, Jafo alitembelea mradi wa barabara ya kuingia Hospitali ya Uhuru katika Halmashauri ya Wilaya Chamwino na kumsisitiza mkandarasi kukamilisha Machi 14, mwaka huu.




Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Brigedia Jenerali John Mbungo (kushoto), akimkabidhi Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi moja ya vitabu vya mwongozo wa taasisi hiyo, wakati wa ufunguzi wa mkutano mkuu wa taasisi hiyo, jijini Dodoma juzi. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Walalamika kutengwa upimaji ardhi, urasimishaji makazi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKAZI wa Mtaa wa Mbwanga, Kata ya Mnadani, jijini Dodoma, wamelalamikia kutoshirikishwa katika upimaji ardhi na urasimishaji makazi katika eneo hilo na kudai kuwapo kwa vitendo vya rushwa kwa baadhi ya watu wasiyostahili kupatiwa viwanja.

Upimaji huo unafanywa na Kampuni ya Geoplan.

Kufuatia hali hiyo, wakazi hao wameiomba Halmashauri ya Jiji la Dodoma kusimamia upimaji huo kwa kuzingatia miongozo na maelekezo ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara, Diwani wa kata hiyo, Paul Bankiye, alisema tangu upimaji uanze hawajawahi kushirikishwa wala kupatiwa mkataba wa upangaji na upimaji.

"Wananchi wangu wamekuwa wakinilalamikia kuwa wanapoomba kupata vibali kwa ajili ya kujenga wananyimwa, lakini baadhi ya watu wanapatiwa vibali na wanendelea kujenga nyumba kama kawaida," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa huo, Solwa Mabuba, alisema hawakushirikishwa katika upimaji huo bali waliona Kampuni ya Geo Plan, ikianza kupima maeneo yao bila ya wao kuelezwa jambo lolote juu ya maeneo yao.

"Hapa tuna kero nyingi kwanza wananchi hatushirikishwi, pia hakuna mkataba wa upangaji na upimaji na vibali vya ujenzi kupata ni shida sasa tunaliomba Jiji la Dodoma watusaidie kwenye hili," alisema.

Akijibu malalamiko hayo, Ofisa Ardhi wa jiji hilo, Leonard Machunda, alisema kero zote zilizojitokeza katika eneo hilo zinatakiwa kutatuliwa katika maeneo ya viwanja na sio ofisini.

"Hapa naona hakuna ushirikishwaji sasa tunatakiwa kukutana site na sio huku ili tujue hizi changamoto za vitendo, lakini pia hakuna kamati ya urasimishaji wa maeneo ambayo ni wananchi hivyo naomba mwenyekiti wa eneo hili kamati hii iundwe," alisema.

Kuhusu, Naibu Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma, Victor Swella, aliwashauri wakazi hao kukaa kwa pamoja na kampuni hiyo ili kutatua kwa vitendo kero zilizopo na kuwataka kutoa taarifa za kuombwa rushwa kama zitajitokeza.

Pia, aliwataka kuwa makini kwenye ulipaji wa viwanja kwa kuwa bei elekezi ni Sh.150, 000 na kuwasisitiza kulipa kwenye mamlaka zinazohusika.



# Mikopo halmashauri sasa kwa vifaa

**Na Grace Mwakalinga,** MBOZI

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, David Silinde, amesema ili kunusuru upotevu wa fedha za serikali, wizara imeelekeza asilimia 10 ya mikopo ya halmashauri kwa vikundi itolewe kwa njia ya vifaa badala ya fedha taslimu.

Silinde alisema hayo jana akiwa mkoani hapa wakati wa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) ambapo alishiriki akiwa mbunge wa Tunduma.

Alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya halmashauri katika Mkoa wa Songwe kushindwa kusimamia ipasavyo urejeshaji wa fedha hizo kutoka kwa wanufaika.

Kutokana na mazingira hayo, alisisitiza kuwa fedha za serikali si hisani bali ni mkopo wenye masharti nafuu unaowawezesha wanufaika kuendeleza shughuli zao za kiuchumi.

Serikali kupitia TAMISEMI imetoa mwongozo mpya wa namna ya kukopesha asilimia 10 ya mikopo ya halmashauri badala ya fedha wameanza kugawiwa vitendea kazi vinavyoendana na thamani ya fedha ambayo wangepatiwa. Nahamasisha watu kutumia njia hiyo kama baadhi ya wilaya zinafanya zikiwamo Lindi na Nachingwea," alisema Silinde.

**Kumekuwa na tabia ya baadhi ya halmashauri katika Mkoa wa Songwe kushindwa kusimamia ipasavyo urejeshaji wa fedha hizo kutoka kwa wanufaika.**

Aliagiza wakurugenzi wote wa halmashauri nchini kusimamia kikamilifu mikopo wanayoitoa na kuacha kuingiza udugu au kufahamisha, hivyo kusababisha fedha hizo kutorejeshwa kwa wakati au kutotumiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

Baadhi ya washiriki wa kikao hicho walisema kuna haja ya kuboresha baadhi ya taratibu za utoaji wa mikopo hiyo ili kuongeza ufanisi kwa wanufaika wa mikopo ambao ni wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Ayubu Mlimba, alisema miongoni mwa njia zitakazosaidia mikopo hiyo kutolewa kwa wakati ni viongozi kuacha upendeleo na maslahi binafsi kwani baadhi yao hunufaika nayo.

Alisema katika halmashauri yake, atahakikisha wale wote wanaodaiwa wanarejesha fedha kwa wakati ili na wengine wapate mikopo ambayo inawanufaisha vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, Jose Msyani, alipongeza serikali kwa kuboresha namna ya utoaji wa mikopo kwa watu wenye ulemavu.

Alisema kwa sasa masharti ya utoaji mikopo kwa Halmashauri imelegezwa ambapo mtu mmoja mwenye ulemavu ambaye anafanya shughuli za ujasiriamali anaweza kupata mkopo bila kuwa kwenye kikundi chochote.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nicodemus Mwangela, alisema baadhi ya halmashauri za wilaya katika mkoa huo zimeshindwa kukusanya marejesho zaidi ya Sh. milioni 800 kwa vikundi vilivyokopeshwa.

Kupitia kikao hicho, aliagiza watendaji wote wa halmashauri kusimamia vyema marejesho ya mikopo waliyoitoa huku akimwomba Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Songwe kufanya uchuguzi kubaini mianya ya rushwa kwenye mikopo hiyo.



Mkulima wa zao la mahindi, Elika Mwakamele wa Kijiji cha Kibisi, wilayani Rungwe, katika Mkoa wa Mbeya, akiwa katika shamba lake wakati wa mavuno, ambapo huvuna kwa kuzingatia uhifadhi ili kukabiliana na kikwazo cha sumu kuvu. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Watakiwa kufuata ushauri wa kitaalam

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

WILAYA ya Chunya imewahimiza wakulima wa Tumbaku kufuata ushauri wa kitaalam kwenye kilimo cha zao hilo ili kuongeza tija ya uzalishaji na kupata faida.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon, wakati akizungumza na wakulima wa Kambikatoto ambapo pamoja na mambo mengine, aliwasisitiza msimu huu wa kilimo kuzingatia ushauri uliotolewa na maofisa ugani ili kupata mavuno mengi na yenye ubora.

" Wilaya ya Chunya ni miongoni mwa maeneo yanayotegemewa kwa uzalishaji wa tumbaku lakini miongoni mwa sababu zinazowakabili wakulima kwa sasa ni ukosefu wa soko la uhakika kuuza zao hilo.

"Kutokana na uhaba wa soko, nawahamasisha msikate tamaa ya kuacha kulima bali ongezeni bidii serikali inaandaa utaratibu mzuri wa kutafuta masoko ili muuze," alisema Simon.

Alisema tumbaku inachangia kwa kiasi kikubwa pato la wilaya kutokana na tozo na ushuru unaotokana na ama kwa kusafirisha au kuuza kwa wafanyabiashara.

Baadhi ya kampuni ambazo zinasambaza mbegu na pembejeo za kilimo wilayani humo, zimesema kuwa zitahakikisha zinafanya mageuzi makubwa kwenye kilimo za tumbaku kwa kuwapatia wakulima mbegu na zana za kisasa.

Mkurugenzi wa Petrobena, Peter Kumalilwa, alisema kampuni yake itabakikisha inatoa mbolea na pembejeo za kutosha ili Wakulima wazalishe kwa malengo na tija katika msimu huu wa kilimo

"Tumejipanga kufanya mageuzi ya kilimo hususani cha tumbaku kwa kuhakikisha wakulima wanapatiwa pembejeo za kilimo na mbegu kwa wakati zikiwamo za kupandia na kukuzia.

## RAS ataja mwarobaini kumaliza uhaba vyumba vya madarasa

**Na Grace Mwakalinga,** MBOZI

SERIKALI mkoani Songwe imehimiza madiwani na watendaji wa Halmashauri kupanga bajeti zitakazotatua uhaba wa vyumba vya madarasa ili kinapofikia kipindi cha wanafunzi kuanza masomo kusiwapo kikwazo.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Songwe, Dk. Seif Shekalaghe, alisema hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe huku akisema njia rahisi ya kukabiliana na tatizo ya vyumba vya madarasa ni wilaya kutenga bajeti mahsusi kujenga huku wakishirikisha wananchi.

Alisema kila mwaka kuna uhaba wa vyumba vya madarasa, hivyo aliagiza wakurugenzi na maofisa elimu kuhamasisha wananchi kuchangia ujenzi wa vyumba vya madarasa pamoja na madawati.

"Kila mwaka kuna uhaba wa vyumba vya madarasa. Naomba suala hili tulishughulikie tuhakikishe tunaweka bajeti ana ya kukamilisha vyumba vya madarasa au madawati huku tukishirikana na wadau pamoja na wazazi," alisema.

Katika hatua nyingine, Dk. Shekalaghe alisema shule zote za msingi na sekondari zianze utaratibu wa kutoa chakula shule ili kuongeza ufaulu na kuimarisha afya za watoto.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nicodemus Mwangela, alisema licha ya shule zote kuanza kutoa chakula shuleni alisisitiza chakula hicho kiwe kizuri kwa ajili ya kurutubisha afya za wanafunzi kwa kuchanganya aina mbalimbali za makundi ya vyakula.

Aliwataka wazazi kuchangia chakula huku akizitaka kamati za shule kuhamasisha ili zoezi hili lianze mara moja.



# Waonywa tamaa kuuza mashamba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Kaskazini 'B' Unguja, Aboud Hassan Mwinyi, amewataka wananchi wa shehia ya Mangapwani kuacha kuuza maeneo yao kwa tamaa ya fedha katika kipindi cha mpito cha kuelekea ujenzi wa bandari.

Akizungumza na wananchi hao huko Mangapwani, alisema katika kipindi hicho cha kuelekea ujenzi wa bandari mbalimbali katika ukanda wa Mangapwani na Bumbwini, watu wengi wamekuwa wakiyataka maeno ya karibu na ujenzi huo ili wahamie katika maeneo hayo.

Alisema kitendo cha kuuza maeneo hayo kwa wakati huu si kitendo kizuri na pia ni kujisababishia ugumu wa maisha, na itafika wakati maeneo ya Mangapwani yatakuwa na gharama kubwa kutokana na uwekezaji.

Akizungumzia kuhusu malipo kwa wananchi watakaoathiriwa na ujenzi wa Bandari, Aboud aliwataka wasiwe na wasiwasi kwa maeneo yaliyoingia katika ujenzi, na kusema kuwa wote watalipwa fidia zao baada ya kufanyiwa utafiti.

Naye Mkurugenzi wa Baraza la Mji la Wilaya ya Kaskazini 'B', Makame Mwadini Silima, akizungumzia mapato yanayokusanywa na baraza la mji, alisema diko la Mangapwani halimo katika sehemu wanayokusanya kiwango kikubwa cha mapato kwa hiyo ni vizuri wananchi wakaachana na migogoro inayojitokeza ambayo kwa kiasi kikubwa inasababishwa na ukusanyaji wa kodi.

Kwa upande wao wananchi wa Mangapwani wakitoa malalamiko yao walisema wanakijiji wanakosa kupata chochote katika fedha zinazoingia kupitia diko lao ambapo kila bamvua (msimu wa samaki) hupatikana kiasi cha Sh. milioni 200.

# Rais Dk. Mwinyi awaita wawekezaji wa Indonesia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewakaribisha wawekezaji kutoka Indonesia kuekeza Zanzibar kutokana na kuwapo mazingira mazuri yaliyowekwa na Serikali yake.

**Zanzibar ina maeneo kadhaa ya kushirikiana na Indonesia hasa ikizingatiwa kwamba nchi hiyo imepiga hatua kubwa kiuchumi.**

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana alipofanya mazungumzo na Balozi wa Indonesia nchini, Prof. Ratlan Pardede alipofika Ikulu kwa ajili ya kujitambulisha. Dk. Mwinyi alisema Serikali imedhamiria kuimarisha uchumi wake, hivyo iko tayari kushirikiana na washirika wengine wa maendeleo ikiwamo Indonesia.

Alisema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Zanzibar zina uhusiano na ushirikiano wa muda mrefu na Indonesia hasa katika uimarishaji wa sekta ambalimbali za maendelo, hivyo, Serikali anayoiongoza imeacha milango yake wazi kwa wawekezaji wa Indonesia kuja kuekeza Zanzibar.

Alisema Zanzibar ina maeneo kadhaa ya kushirikiana na Indonesia hasa ikizingatiwa kwamba nchi hiyo imepiga hatua kubwa kiuchumi.

Akieleza kuhusu sekta ya uwekezaji, alisema Zanzibar iko tayari kuwakaribisha wawekezaji kutoka Indonesia kuja kuwekeza katika sekta ya bandari ukiwamo mradi ambao umo kwenye upembuzi yakinifu wa Bandari ya Mangapwani/Bumbwini utakapokuwa tayari kuanza.

Pia Rais Dk. Mwinyi alimueleza Balozi huyo kwamba mbali ya uwekezaji katika sekta hiyo pia, kutokana na nchi hiyo kupata maendeleo makubwa katika sekta ya utalii, Zanzibar inawakaribisha wawekezaji katika sekta hiyo kuja kuekeza nchini.

Alieleza Zanzibar imejaaliwa kuwa na vivutio kadhaa vya utalii, hivyo milango yake iko wazi kwa wawekezaji wa sekta hiyo kutoka Indonesia kuja kuwekeza.

Aidha, aliipongeza Indonesia kwa kufungua kiwanda cha kusarifu majani makavu na yaliyoanguka yenyewe ya mkarafuu kilichopo Mgelema, Chake Chake Mkoa wa Kusini Pemba.

Hivyo, alieleza haja kwa Indonesia kujenga kiwanda cha mwani hapa Zanzibar hasa ikizingatiwa kwamba bidhaa hiyo inalimwa kwa wingi Zanzibar, lakini bado wakulima wake hajanufaika na bei ya zao hilo sambamba na kutokuwapo kwa soko la uhakika.

Naye Balozi Prof. Pardede alisema Serikali yake itaendelea kuiunga mkono Zanzibar katika kuimarisha uchumi wake ikiwamo kuitangaza zaidi Zanzibar kwa wawekezaji wa Indonesia.

Aidha, Balozi Pardede alimpongeza Rais Dk. Mwinyi kwa mwanzo mzuri aliouonyesha katika uongozi wake sambamba na kuonekana kwa mwanga wa matumaini na mafanikio makubwa katika siku mia moja za uongozi wake.



Mstahiki Meya wa Jiji la Zanzibar, Mahmoud Mohammed Mussa, akizungumza wakati akizindua baraza la jiji hilo, Shangani Mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kamati kusimamia majukumu ya jiji Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BARAZA la Jiji la Zanzibar limezindua kamati mbalimbali zitakazosimamia utekelezaji wa majukumu ya baraza hilo ili kufikia malengo ya kuanzishwa kwake.

Akizungumza katika uzinduzi huo uliofanyika jana katika ofisi za baraza hilo Shangani, Meya wa Jiji la Zanzibar, Mahmoud Mohammed Mussa, alisema kuwapo kwa kamati hizo kutaondosha mwingiliano wa majukumu kati ya baraza la Jiji na manispaa zilizopo nchini.

Alizitaja kamati hizo kuwa ni ya sheria na utawala kamati hizo pamoja na kamati ndogo ya kuangalia majukumu ya baraza la jiji kisheria kupitia sheria iliyopo.

Alisema sheria namba Saba ya mwaka 2014 ya sheria ya mamlaka za serikali za mitaa pamoja na marekebisho ya sheria hiyo yaliyofanywa mwaka 2020, yalibaini mwingiliano wa kazi za mabaraza ya Manispaa na Jiji.

"Kuanzisha kamati hizi kutatusaidia kufanya shughuli zetu bila ya mivutano na mabaraza yetu ya manispaa yaliyomo katika Mkoa wa Mjini Magharibi hususani katika ukusanyaji wa mapato katika vyanzo mbalimbali," alisema Mahmoud.

Aidha, aliwataka wajumbe hao kuanza kazi haraka na kutengeneza mikakati imara ya vyanzo vya mapato ambavyo vitaweza kuchangia baraza hilo kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo.

"Wajumbe lazima sasa tuongeze ubunifu na kuibua vyanzo vipya vya mapato ambavyo manispaa zetu hazikusanyi kama vile maeneo ya visiwa, hoteli kubwa, miradi mikubwa ya ujenzi iliyomo katika jiji, utalii na nyenginezo," alisema Mahmoud.

Mahmoud aliwaagiza wajumbe wa baraza hilo ambao ni madiwani, kuhakikisha wanasimamia kikamilifu suala la usafi katika maeneo ya jiji hilo na kuondokana na utamaduni wa kusimamiwa katika utekelezaji wa majukumu yao.

Kwa upande wao wajumbe wa baraza hilo, walisema watafanyakazi kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo ili kurejesha imani kwa jamii na kuona umuhimu wa kuwapo kwa Jiji la Zanzibar.

Kamati zilizozinduliwa na wajumbe wa baraza hilo ni Kamati ya Fedha na Bajeti ambayo inaongozwa na Meya Mahmoud Mohamed Mussa, Kamati ya ufundi na mipango Mjini inayoongozwa na Diwani wa kuteuliwa, Aboud Hassan Serenge, wakati Diwani Janeth Norah Sekihola, akiongoza kamati ya sheria na utawala.

Kamati nyingine ni huduma za jamii, itakayoongozwa na Abdul-Latif Omar Haji na kamati ya kusimamia kamati ndogo ya utendaji na majukumu ya baraza la Jiji la Zanzibar kisheria inayoongozwa na Rahma Ali Khamis.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**James L. Saitabau** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne Chenye namba **S.2907-0144** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kwa mtihani wa mwaka 2013 katika shule ya Sekondari Olokii. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi namba **IRI/IRI/RB/79117/2021.**

## TANGAZO LA MNADA/NOTISI

**SEPCO DEBT COLLECTION & AUCTIONEERING CO. LTD** kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD** tunatoa notisi ya madai ya siku kumi na nne (14) kwa ndg **Amina Martin Bagule** ambaye ni mdaiwa sugu kuwa uwe umelipa deni lako unalodaiwa na Tujijenge Tanzania Ltd pamoja na gharama zote za dalali tangu siku ya tangazo hili gazetini.

Kushindwa kulipa tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara Shamba lenye nyumba uliyoweka dhamana ya mkopo iliyopo Kimara –Mtaa wa King'azi kwa mujibu wa sheria. Mnada utafanyika tarehe **27.03.2021** kuanzia saa nne (4) asubuhi mara baada ya gari la matangazo kupita sehemu mali husika ilipo.

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalipa 25% siku ya mnada na 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa salio halirudishwi na mnada utarudiwa.
2. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**0715683777/0712670704/0713052578 au**
**Email: info@sepcoauctioneering.co.tz**

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD, SEPCO DEBT COLLECTION & AUCTIONEERING CO. LTD** tutauza kwa mnada wa hadhara gari la mdaiwa Sugu, mali ya Ndugu **NAYAZ NIAZIM BHANJI (T 942 DEF- TOYOTA NOAH).** Gari lipo katika yard ya Makumbusho.

Lengo ni kufidia/ kupunguza deni la mkopo analodaiwa. Mnada utafanyika Tarehe **20/03/2021,** mahali dhamana ilipo. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi.

Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**0715683777/0712670704/0713052578**
**Email: info@sepcoauctioneering.co.tz**

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi NO.62/2021**

**Ombi la FATUMA SHABANI SELEMANI kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu MOHAMEDI JUMA TEMBO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 16/03/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 03/03/2021

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi NO.61/2021**

**Ombi la ELIAS HASSAN MWAKALUKWA kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu LIDE HASSAN MWAKALUKWA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 08/04/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 03/03/2021

## NAFASI ZA KAZI

### Secretary

Tunahitaji Secretary mzoefu mwenye customer care.

**Sifa:**
**Umri:** miaka 25 hadi 35
**Elimu:** kidato cha nne na kuendelea
Awe ana basic computer skills na uzoefu wa kazi wa zaidi ya miaka miwili.

**Namba zetu za simu ni 0625 741821.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MBEYA**

**MADAI NO.31/2020**

**ASHA GODWIN LWIBA................................MDAI**

**DHIDI YA**

**SAID JAPHARI JOKA.......................................MDAIWA**
**DALBIT PETROLEUM TZ LTD.........................MDAIWA**
**RELIANCE INSURANCE CO LTD (T)................MDAIWA**
**MILMAR CONSULTANTS LTD.........................MDAIWA**

**Kwa:SAID JAPHARI JOKA**
**POPOTE ALIPO**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA.**

Unataarifiwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya au wakili wako mnamo tarehe 08/03/2021 siku ya Jumatatu saa 3:00 asubuhi,ambapo shauri limepangwa kusikilizwa.

ELEWA KWAMBA.Ukikosa kufika siku hiyo shauri hili litasikilizwa bila wewe kuwepo na uamuzi kutolewa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 11 mwezi 02,mwaka 2021.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DODOMA**

**MAOMBI YA SHAURI LA ARDHI NA.12/2019**

**NEEMA TUWA ABDALLAH (Suing as admistratrix of the state of TUWA ABDALLAH TUWA.........MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**CRDB BANK PLC AND 5 OTHERS......MJIBU MAOMBI**

**KWA CAPITAL ZOO AUCTION MART AND COURT BROKERS**

**POPOTE ULIPO**
**YAH: TAARIFA YA KUSIKILIZWA KWA MAOMBI YA SHAURI LA ARDHI NA.12/2019 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA-DODOMA**

UNAFAHAMISHWA KWAMBA; shauri tajwa hapo juu litasikilizwa Mahakama Kuu ya Tanzania,kanda ya Dodoma,mbele ya MHE.JAJI M.M.SIYANI, wa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma,saa tatu (3:00) kamili asubuhi siku ya jumatano tarehe 14/4/2021.

**HIVYO;** Mnatakiwa mfike nyinyi wenyewe au Wakili wenu siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.

**NA ENDAPO;** Hamtafika nyinyi wenyewe au wakili wenu siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itavyoamua pasipo nyinyi au Wakili wenu kuwepo.

**IMETOLEWA;** kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama leo hii tarehe 21/01/2021.

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**ANNA CHRISOSTOM BUHATWA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA **NOAH** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 457 CGE.** KADI YA GARI AINA YA CELSIOR YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 927 ANL.** YOYOTE ATAKAYEZIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI:
**DAR/OST/RB/79089/2012.**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF ILALA**
**AT KINYEREZI**

**CIVIL CASE NO 74 OF 2020**

**LEISURE TOURS AND HOLIDAYS LTD ... ... PLAINTIFF**

**VERSUS**

**SYMBION POWER TANZANIA LTD.....DEFENDANT**

**NOTICE OF EX-PARTE JUDGEMENT**

**The NOTICE** that the above case has been fixed for EX PARTE JUDGEMENT

On the 5TH DAY OF MARCH 2021 at 10:00am Before Hon MPAZE SRM

You are required to appear in court without fail in which Ex-Parte Judgment will

Be delivered by the Court.

Given under my hand and seal of the court this 3rd day of March 2021

**SENIOR/RESIDENT MAGISTRATE**

**COPY TO BE SERVED UPON**
**SYMBION POWER TANZANIA LTD**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA**
**KINONDONI**

**SHAURI LA MIRATHI NA. 25 YA 2021**

**Maombi ya barua ya Usimamizi wa Mirathi ya Marehemu**
**ANNA LIONEL MAWALLA...................MAREHEMU**

**NA**

**SEPI LIONEL MAWALLA....................MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanaofahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 16 Mwezi wa 03 mwaka 2021.

Hati hii imetolewa tarehe 02 Mwezi wa 03 Mwaka 2021.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA: 52/2021**

**MDAI: FREDY TIMOTHY KILIMA**

**DHIDI YA**

**MDAIWA: 1. EMANUEL JUSTINO MWIPOPO NA**
**2. FAUSTIN M. MASAWE**

**KWA: EMANUEL JUSTINO MWIPOPO**

**Ombi la mdai FREDY TIMOTHY KILIMA**
**Madai ya PESA TSHS. 2,272,000/=**
**GHARAMA TSHS. 15,000/=**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa. Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 9 Mwezi wa 3 Mwaka 2021 saa 2:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 23 Mwezi wa 02, 2021.

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Wanasayansi mbioni kupata dawa UKIMWI

**Kinshasa, DRC**

WANASAYANSI wanaamini kwamba huenda wanakaribia kupata tiba ya Virusi Vya Ukimwi (VVU), baada ya matokeo ya utafiti kutolewa juzi.

Utafiti umebaini wapo watu wanaoweza kudhibiti VVU nchini DRC, bila kutumia dawa.

VVU viligunduliwa DRC miongo minne iliyopita.

Utafiti ulitathmini sampuli zilizokusanywa 1987 na 2019 na kubaini kwamba asilimia nne ya watu wanaoishi na VVU DRC, waliweza kukandamiza kiwango cha virusi hadi kufikia kiwango cha chini zaidi bila kutumia dawa.

Kulingana na mwandishi wa BBC, Rhoda Odhiambo kwa miaka kadhaa sasa wanasayansi wameendelea kufanya kazi ya kutafuta kinga ya VVU.

Utafiti mpya uliofanywa na kampuni ya afya kwa jina Abbott, umewapatia tabasamu wanasayansi, hususan kuhusu kundi dogo la watu kwa jina Wadhibiti wa VVU (HIV Controllers).

Pia utafiti umegundua virusi vya ugonjwa huo vinakandamizwa kwa kutumia jeni za watu hao zisizo za kawaida.

Ulibaini idadi ya watu wanaoishi na VVU nchini humo, kati ya 1987 hadi 2019, asilimia nne walikuwa na uwezo wa kudhibiti virusi hivyo.

Dk. Mary Rodgers, kiongozi wa utafiti huo aliiambia BBC kwamba wanasayansi tayari wanajua kuhusu kundi hilo, ingawa hawajawahi kuona viwango kama hivyo vya juu katika taifa moja.

Pia ilibainika asilimia moja ya watu wanaoishi na VVU nchini Cameroon pia wana uwezo huo.

Kwa sasa watu wanaoishi na VVU hulazimika kutumia dawa kila siku, ili kuafikia uwezo huo.

Dk. Rodgers alisisitiza umuhimu wa kufanya utafiti zaidi kuhusu idadi ya watu na katika mataifa mengine, baada ya utafiti wa awali kuonyesha kwamba watu wanaweza kupoteza kinga huku ugonjwa huo ukiendelea kuwaathiri.

Kutokana utafiti huo, wanasayansi wanaamini kwamba taifa hilo linaweza kuwa na majibu kudhibiti ugonjwa huo uliowaathiri wanawake walio na umri mdogo na wasichana katika eneo la Jangwa la Sahara, barani Afrika.

***BBC***



Waandamanaji waliojitokeza barabarani kupinga mapinduzi ya kijeshi wakikimbia mabomu ya kutoa machozi yaliyorushwa na polisi, mjini Mandalay, Myanmar, jana. **PICHA/AP**

## WHO: Watu bilioni 2 kupoteza usikivu

**Newyork, MAREKANI**

RIPOTI mpya ya Shirika la Afya Duniani (WHO) limetahadharisha kuwa ifikapo mwaka 2050 takribani watu bilioni 2.5 watapoteza uwezo wao wa kusikia.

Ripoti ilionyesha nchi zenye kipato cha chini, kwa asilimia 78 zina wataalamu wachache wa masikio, pua na koo, (ENT).

Pia ilibainika kila mtaalamu mmoja anatumika kwa idadi ya watu milioni moja.

Ikiwa jana ni Siku ya Usikivu Duniani, WHO limesema ikiwa hatua hazitachukuliwa mapema, kiwango kikubwa cha watu kitaishi katika hali hiyo.

Idadi hiyo ya watu iliyotajwa na ripoti ya WHO, ni sawa na mtu mmoja kati ya watu wanne, atakuwa anakabiliwa na tatizo la usikivu.

Lilisema, takribani watu milioni 700, watahitaji kutumia vifaa vya kusikilizia au tiba ya masikio na huduma nyingine za kurekebisha masikio yao.

Ripoti ilisema ukosefu wa taarifa sahihi na mitazamo ya unyanyapaa kwa magonjwa ya masikio na upotezaji wa usikivu mara nyingi huzuia watu kupata huduma dhidi ya hali hizi.

Pia takwimu kwa nchi nyingine kwa asilimia 93 wana chini ya mtaalamu mmoja wa sauti anayeshughulikia usikivu wa masikio kwa watu milioni moja na nchi zingine kwa asilimia 50 wana mwalimu mmoja wa viziwi, kwa viziwi milioni moja.

WHO linasema pengo hilo linaweza kuzibwa kupitia ujumuishaji wa huduma ya masikio katika huduma ya msingi ya afya.

Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Dk. Tedros Ghebreyesus alinukuliwa akisema, "uwezo wetu wa kusikia ni wa thamani. Upungufu wa kusikia usiotibiwa unaathari mbaya kwa watu kuwasiliana, kusoma na kipato. Inaathiri afya ya akili na uwezo wao wa kudumisha uhusiano."

***UN***

## Chama cha Bobi Wine chadai raia 458 kupotea

**Kampala, UGANDA**

CHAMA cha National Unity Platform (NUP), kimesema takriban raia 458 wa Uganda hawajulikani walipo na hakuna taarifa zozote zinazofahamika kuwahusu.

Hata hivyo, gazeti la Daily Monitor limeripoti kwamba nakala ya orodha ya watu wasiojulikana walioshuhudia ya Chama cha NUP ni watu 243.

Awali, Spika wa Uganda, Rebecca Kadaga, alisema serikali imechukua muda mrefu kujibu agizo la bunge la kutaka iweke wazi majina ya watu wasiojulikana walipo.

Kadaga alisema serikali itawajibishwa kuhusiana na taarifa za watu waliopotea kwa sababu imeshindwa kuweka wazi orodha yao mbele ya umma, kulingana na gazeti la Daily Monitor.

"Tangu kikao cha kwanza cha bunge kilichohudhuriwa na kila mmoja, kumekuwa na malalamiko juu ya madai ya watu wasiojulikana walipo. Rais aliagiza walio na majina ya watu hao kuyachapisha," Spika huyo alisema.

"Kwa kuwa orodha hiyo bado haipo, natoa wito kwa walio na orodha hiyo yenye majina ya watu wasiojulikana walipo kuitoa hapa, ili serikali iweze kuwajibishwa."

Uamuzi wake unafuatia ombi la Mbunge wa Kalungu Magharibi, Joseph Ssewungu, aruhusiwe kuweka wazi orodha ya watu hao.

Inadaiwa kwamba watu hao walitekwa nyara na maofisa wa usalama waliokuwa wanashika doria kwa kutumia magari aina ya Toyota Hiace, ambayo ni maarufu kwa wenyeji kama magari yasiyo na rubani yaani drones.

**BBC**

## Majimbo USA yaondoa sharti kuvaa barakoa

**Washington, MAREKANI**

TEXAS itaondoa hitaji la watu kuvaa barakoa na kuruhusu biashara kufunguliwa, kuanzia wiki ijayo.

Gavana Greg Abbott alitangaza agizo hilo na kwamba litaanza kutekelezwa Machi 10, mwaka huu.

Alisema agizo hilo, linaondoa mahitaji yote ya kuvaa barakoa na linazuia mamlaka kuwaadhibu wakazi wasiovaa barakoa.

Pia agizo linaondoa vikwazo vya kibiashara zilizo kwenye kaunti ambazo hazina idadi ya juu ya wagonjwa wa Covid-19 hospitalini.

Texas ndio jimbo kubwa la Marekani kutamatisha uhitaji wa kuvaa barakoa.

Tangazo hilo la Texas limetokea huku majimbo mengine yakiwamo Michigan, Louisiana na Mississippi kuchukua hatua kama hiyo ya kufutilia mbali mahitaji ya watu kuvaa barakoa.

**BBC**

# KOEMAN

## ACHIMBA MKWARA BARCELONA



**BARCELONA, Hispania**

RONALD Koeman amezungumzia uvumi unaoendelea juu ya majaliwa yake kwenye dimba la Camp Nou, akisisitiza Barcelona "watapata shida" kama ataondoka.

Koeman alipewa mkataba wa miaka miwili na Barca wakati alipochukua nafasi ya Quique Setien katikati ya Agosti, mwaka jana, lakini sasa anajikuta akipata presha kwa msimu huu 2020-21.


Uvumi unadai raia huyo wa Uholanzi anaweza kupoteza kazi yake wakati rais ajaye wa klabu atakapochaguliwa baadaye mwezi huu, na sasa amekiri kutokuwa na uhakika kama atapewa nafasi ya kubaki hadi mwaka 2022.

"Sijazungumza na mtu yeyote. Tunapaswa kusubiri ni nani atakayekuja kama rais na mpango wake," alisema Koeman alipozungumka katika mkutano wa waandishi wa habari.

"Ikiwa sioni wakati muhimu kwangu tutakuwa na shida, kwa sababu nina mwaka mmoja zaidi kwenye mkataba wangu."

Barca pia wako kwenye hatihati ya kutupwa nje kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya kupoteza mchezo wa kwanza wa hatua ya 16 dhidi ya Paris Saint-Germain kwa kufungwa mabao 4-1.

## Scholes amtaka Alcantara kutua United



**MANCHESTER, England**

GWIJI wa Klabu ya Manchester United, Paul Scholes anaamini nyota mpya wa Klabu ya Liverpool, Thiago Alcantara angefanya vizuri ikiwa angekuwa ndani ya dimba la Old Trafford.

Thiago sio aina ya wachezaji ambao wanafiti kwenye mfumo wa Kocha, Jurgen Klopp jambo ambalo linamfanya ashindwe kwenda na kasi ya kikosi hicho ambacho kinatetea taji la Ligi Kuu England.

Hiyo ni kwa mujibu wa Scholes ambaye amesema kuwa kwa namna alivyomtazama nyota huyo, wengi wanamlaumu bila kujua kwamba anatumika tofauti na uwezo wake.

Ameweka wazi kwamba, alianza kumtazama Thiago tangu anatua ndani ya kikosi cha Liverpool baada ya kujiunga hapo akitokea Klabu ya Bayern Munich.

"Ni kiungo mzuri naona kwamba wengi wanamlaumu kutokana na kushindwa kuonyesha uwezo wake, lakini anashindwa kwa sababu bado sio aina ya wachezaji wa Klopp.

"Kwa namna ambavyo Liverpool wanacheza mbele wakiwa watatu inakuwa ngumu kwake kwenda mbele zaidi na anakuwa chini na haonekani hivyo bado mtindo wa Liverpool unamkataa.

"Nadhani labda angekuwa ndani ya Manchester United angepata nafasi ya kuwa imara na bora zaidi ila kwa sasa ni jambo la kusubiri."

## Koulibaly aonyeshwa kadi nyekundu ya saba

**NAPLES, Italia**

KALIDOU Koulibaly amepata adhabu ya kufungiwa mechi moja na alikosa mchezo wa Napoli wa Serie A jana Jumatano dhidi ya Sassuolo, baada ya kuonyeshwa kadi yake ya saba nyekundu kwenye maisha yake ya soka.

Mlinzi huyo wa kati mwenye umri wa miaka 29 alipewa kadi mbili za njano zilizozaa nyekundu katika ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Benevento, Jumapili.

Beki huyo raia wa Senegal amesimamishwa na hakuhusika wakati vijana wa kocha, Gennaro Gattuso walipocheza na Sassuolo.


Mlinzi huyo ametolewa kwa kadi nyekundu mara saba katika maisha yake ya soka, akipokea kadi yake ya kwanza nyekundu mwaka 2011 wakati akiichezea Metz dhidi ya Clermont.

Koulibaly alipata kadi nyingine nyekundu wakati wa mchezo wa Napoli dhidi ya Sampdoria mwaka 2014, na dhidi ya Fiorentina mwaka 2018.

Alitolewa nje mara mbili mwaka 2019 na alipokea kadi nyekundu wakati Senegal ilipomenyana na Burkina Faso mwaka 2017, wakati wa kufuzu fainali za Kombe la Dunia la 2018.

Mchezaji huyo pia alisimamishwa katika fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika ya Senegal dhidi ya Algeria, ambapo walishindwa na Mbweha hao wa Jangwani na wakamaliza kwenye nafasi ya pili katika mashindano hayo.

Ameichezea Napoli mechi 28 msimu huu 2020-21, akiwasaidia kufikia nafasi ya sita msimamo wa Ligi Kuu Italia.





# CHELSEA YAJITOSA KWA DONNARUMMA

**LONDON, England**

CHELSEA inamfuatilia kwa karibu golikipa wa AC Milan, Gianluigi Donnarumma ambaye mkataba wake unakaribia kufikia mwisho pale kwenye dimba la San Siro, kwa mujibu wa Eurosport.

Majaliwa ya Donnarumma na miamba hao wa Serie A, Milan yako mbali na anajiandaa kuwa mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu.

Huku tayari Chelsea ikiwa na makipa, Edouard Mendy na Kepa Arrizabalaga kwenye kikosi chao, miamba hao wa Ligi Kuu England wameripotiwa kumwania Donnarumma.

Mkataba wa golikipa huyo unamalizika mwishoni mwa msimu huu na Milan wamekuwa wakijaribu kumshawishi kusaini mkataba mpya, lakini nyota huyo wa kimataifa wa Italia bado hajafikia uamuzi wa kukubali.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 tayari amekuwa akihusishwa na klabu kama Manchester United, Juventus, Bayern Munich na Paris Saint-Germain.

# VAZQUEZ AITUNISHIA MSULI REAL MADRID

**MADRID, Hispania**

NYOTA wa Real Madrid, Lucas Vazquez ameionya klabu hiyo kwamba, hatasubiri kwa muda mrefu kwa wao kufikia mahitaji anayoyataka kwenye mkataba mpya.

Winga huyo mwenye umri wa miaka 29, mkataba wake wa sasa utamalizika mwishoni mwa msimu huu na mazungumzo kuhusu mkataba mpya yamekuwa yakisuasua.

Vazquez amebakia kuwa mchezaji muhimu kwa kikosi cha Zinedine Zidane akianza katika mechi 23 kati ya 26 msimu huu, na kwa mujibu wa ABC, anataka kuongezewa mshahara katika mkataba wake mpya.

Anataka kuongezwa asilimia 15 katika mshahara mpya, huku Real wakiwa hawapo tayari kufanya hivyo.

Badala yake wanamtaka Vazquez kupunguza ongezeko hilo la mshahara hadi asilimia 10, kwani klabu ipo kwenye hali mbaya kiuchumi baada ya mlipuko wa virusi vya corona.

# GUARDIOLA: BARCA ITARUDI KWENYE UBORA

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola ana matumaini "klabu bora duniani" Barcelona itarudi kwenye kiwango chake "kwa kipindi cha muda mfupi" chini ya rais mpya.

Rais wa zamani wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu baada ya kushikiliwa na polisi kwa siku moja kwa makosa ya "rushwa na matumizi mabaya ya ofisi" aliachiwa juzi.

Bartomeu na Mkurugenzi wa zamani, Jaume Masferrer walisomewa mashtaka hayo Jumanne na kutakiwa kutojibu chochote.

Kocha na mchezaji wa zamani wa Barca, Guardiola anaamini mambo yatatulia ndani ya klabu hiyo ya Katalunya mara baada ya uchaguzi wa urais unaofanyika Jumapili hii.

Katika uchaguzi huo, wagombea watatu wanawania nafasi ya urais ambao ni pamoja na Joan Laporta, Victor Font na Antoni Freixa.

Akizungumza baada ya ushindi wa Manchester City wa 4-1 dhidi ya Wolves kwenye Ligi Kuu England, Jumanne, Guardiola alisema: "Najua hali si nzuri kwa sasa na nina matumaini watamaliza salama.

"Yeye (Bartomeu) kwa sasa bado hana hatia hadi pale atakapopatikana na hatia.

"Kwa upande wangu mimi, klabu bora duniani Barcelona itarudi kuwa imara sana kwa kipindi cha muda mfupi mara tu watakapopata rais mpya."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO AFUNGUKA KUPENDA MASUMBWI

Mshambuliaji huyo alisema pia mchezo huo unasaidia kukuza hisia na kujifunza kusonga...

**TURIN, Italia**

NYOTA wa Juventus, Cristiano Ronaldo amesema anapendelea sana kutazama ndondi kuliko mechi za mpira wa miguu.

Ronaldo ni mmoja wa wachezaji wakubwa wa mpira wa miguu wa wakati wote duniani baada ya kuzichezea klabu za Real Madrid, Manchester United, Juventus na Timu ya Taifa ya Ureno.

Mshindi mara tano wa Ballon d'Or ndiye mfungaji bora mwenye rekodi kwa Real Madrid, wakati tuzo zake ni pamoja na mataji matano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, mataji matatu ya Ligi Kuu England, Euro 2016, mataji mawili ya Serie A na ushindi mwingi huko LaLiga.

Lakini linapokuja suala la kutazama runinga, Ronaldo amesema upendo wake yeye ni kwenye michezo ya kupigana.

"Kucheza mpira wa miguu ni mapenzi yangu, lakini napendelea kutazama michezo mingine kwenye runinga," alisema Ronaldo akimwambia nyota wa ndondi, Gennady Golovkin katika mahojiano kupitia DAZN.

Ronaldo, ambaye amewahi kukutana na nyota wa mchezo huo, Conor McGregor hapo awali, aliongezea: "Nilipokuwa Manchester United, kocha alifanya mazoezi ya ngumi na mimi.

"Nadhani kufanya mazoezi ya ndondi ni muhimu kwa mpira wa miguu, kwa sababu kunakuza hisia zako na unajifunza kusonga."

Ronaldo alisherehekea mechi yake ya 100 ya Juventus kwa kufunga katika ushindi wa 3-1 Serie A Jumapili dhidi ya Genoa.

Sio tu kwamba Ronaldo alikuwa akicheza mechi yake ya 100 ya Juve, pia alikuwa mchezaji wa kwanza kupata ushindi wa 400 katika ligi tano bora za Ulaya karne hii.

## KWA UFUPI

**VARANE ANUKIA UNITED**

REAL Madrid ipo tayari kumuuza mlinzi wake wa kati, Raphael Varane kwa Manchester United baada ya kuthibitisha kwamba, nyota huyo mwenye umri wa miaka 27 hatasaini mkataba mpya hapo kwenye dimba la Bernabeu. ***(Manchester Evening News)***

**DONNARUMMA SOKONI**

CHELSEA inamfuatilia kwa karibu golikipa wa Italia na AC Milan, Gianluigi Donnarumma mwenye umri wa miaka 22 ili kuweza kumsajili kama hatasaini mkataba mpya na miamba hao wa Serie A club. ***(Eurosport)***

**TUCHEL AMTAKA HOFMANN**

KIUNGO wa Borussia Monchengladbach na Ujerumani, Jonas Hofmann mwenye umri wa miaka 28, amedokeza kwamba, kocha wa sasa wa Chelsea ambaye alimnoa wakati akiwa Borussia Dortmund, Thomas Tuchel anataka kumsajili. ***(Ruhr Nachrichten via Mail)***

**LAPORTA AITISHA BARCA**

MGOMBEA urais wa Barcelona, Joan Laporta amesema fowadi wao raia wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33, ataondoka klabuni hapo kama yeye hatashinda uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Machi 7, mwaka huu. Mkataba wa sasa wa Messi unamalizika kipindi cha majira ya joto. ***(Marca)***

**MISHAHARA KUPUNGUZWA**

KLABU za Barcelona na Atletico Madrid zimeamuliwa kupunguza mishahara ya wachezaji wake, kutokana na athari za kiuchumi baada ya mlipuko wa virusi vya corona. ***(Sun)***

**LEEDS: RAPHINA HAONDOKI**

LEEDS United inapanga kumbakisha winga wake, Raphinha mwenye umri wa miaka 24, huku akiwa anawaniwa na klabu za Manchester United na Liverpool. ***(Mirror)***

**NI HAALAND, MBAPPE**

MANCHESTER United inatakiwa kufanya kila jitihada kumsajili straika wa Borussia Dortmund, ~~Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20~~ au fowadi wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22, amesema mlinzi wa zamani wa mashetani wekundu hao, Rio Ferdinand. ***(Mirror)***

**EN-NESYRI KUMRITHI HAALAND**

KLABU ya Borussia Dortmund inawania kumsajili straika wa Sevilla raia wa Morocco, Youssef En-Nesyri mwenye umri wa miaka 23, ili kuziba pengo la Erling Haaland kama ataondoka. ***(Eurosport)***

**SOUTHGATE: TUTAFURAHIA**

KOCHA wa Timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate amesema "litakuwa jambo la kushangaza na kufurahishwa kwa kila mmoja" kama Uingereza na Ireland watashinda nafasi ya kuandaa Kombe la Dunia mwaka 2030. ***(Talksport)***

**EDOUARD ANUKIA ARSENAL**

ARSENAL imemuulizia straika wa Celtic mwenye umri wa miaka 23 raia wa Ufaransa, Odsonne Edouard. ***(Transfer Window Podcast, via Football London)***

**VILLA YAMTAKA BARKLEY**

ASTON Villa haina uhakika kama itamshawishi kiungo, Ross Barkley mwenye umri wa miaka 27 anayecheza kwa mkopo kutoka Chelsea kusaini mkataba wa kudumu klabuni hapo. ***(Football Insider)***

HABARI MICHEZO

# JKT TANZANIA YAJIPANGA HUKU IKIIOMBEA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Simba ikiondoka nchini na kuelekea Sudan kwa ajili ya mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Merrikh, Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Mohamed Abdallah 'Bares' amesema anawatakiwa kila la kheri Wekundu wa Msimbazi kwa sababu wanaenda kuiwakilisha nchi.

Kocha huyo ametoa kauli hiyo ikiwa ni siku chache tangu kikosi chake kilipopokea kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa Simba katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Bares alisema kama Mtanzania anaitakia timu hiyo ifanye vyema kwa sababu kitendo cha kufanya vizuri kitasaidia nafasi ya timu za kushiriki katika mashindano ya kimataifa ziongezeke na kuleta ushindani kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Bares alisema endapo Simba itazidi kung'ara, uhakika wa Tanzania kutoa timu nne msimu ujao utakuwa mkubwa na hivyo ushindani kwenye Ligi Kuu utaongezeka kwa ajili ya klabu kusaka nafasi ya kushiriki michuano hiyo ya kimataifa.

"Mimi kama Mtanzania nawatakiwa kila la kheri Simba kwa sababu mafanikio yao ni mafanikio ya nchi na soka la Tanzania, kwa sababu huenda timu zikaongezea na ikiwa hivyo, basi hata ligi yetu itakuwa na ushindani mkubwa wa kutafuta kumaliza kwenye nafasi za juu," alisema Bares.

Akiizungumzia Simba, Bares alisema ni ukweli usiopingika kuwa timu hiyo ina wachezaji wa kigeni wenye uwezo mkubwa wa kuamua matokeo ya mechi au kufanya kitu tofauti ukilinganisha na nyota wazawa.

"Mimi ni muumini wa wazawa, lakini ukweli lazima tuseme mchezaji wa kigeni ni wa kigeni tu, hawa wachezaji wa Simba baadhi yao wana uwezo binafsi, zaidi ya ule ambao wanafundishwa na kocha, na hiyo inawafanya wawe bora," alisema kocha huyo.

Aliongeza kikosi chake kitafanyia kazi upungufu uliyojitokeza kwenye mechi dhidi ya mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara ili kurejea uwanjani katika mchezo unaofuata wakiwa imara.

Alisema mpaka sasa hakuna timu yenye nafasi ya kutwaa ubingwa au kushuka daraja, hivyo bado ligi hiyo ina ushindani.

"Nafasi zote hazina mwenyewe, tumeingia kwenye mzunguko wa kukamilisha hesabu, tunaamini nasi tutafanikiwa kufikia malengo, ligi imezidi kuwa ngumu na hakuna timu inayojiamini kabla ya filimbi ya mwisho kupilizwa," alisema.

Kikosi cha JKT Tanzania kimeendelea kubakia jijini na Jumapili kitaelekea kwenye Uwanja wa Mabatini Mlandizi mkoani Pwani kuwafuata wenyeji Ruvu Shooting.




Mlezi wa mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Simba Queens, Fatema Dewji (kulia), akimkabidhi jezi na kumkaribisha msemaji mpya wa timu hiyo, Yvonne Cherry 'Monalisa' baada ya kumtangaza rasmi kushika nafasi hiyo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MTANDAO**

# Kaze awatetea Sarpong, Nchimbi

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze amewatetea wachezaji wake, Michael Sarpong na Ditram Nchimbi kwa kusema suala la kutofunga ni tatizo la mfumo mzima na wala wasitupiwe lawama.

Kaze alisema hayo kutokana na baadhi ya wanachama na mashabiki wa Yanga kuwashutumu wachezaji hao ambao mara nyingi wameonekana wakipoteza nafasi za wazi katika mechi mbalimbali wanazopangwa.

Kocha huyo raia wa Burundi alisema ni kweli kama washambuliaji wanakosa mabao au hawafungi ni lazima mashabiki wawaseme au kuwakosoa, lakini anavyoona yeye tatizo ni la uchezaji kuanzia nafasi ya viungo, jinsi anavyotengeneza nafasi, mikimbio na kuwalisha washambuliaji hao.

"Kuna tatizo, lakini si la kwao peke yao. Hili tunalibeba na tunalifanyia kazi na nadhani litarekebishika. Kinachotakiwa ni wanawachezesha na kutengeneza nafasi, mikimbio yao iwe vipi, sehemu gani ya kupenyeza mipira, au kupiga pasi za mwisho, hapa ndipo panatakiwa kuanza kuangaliwa kabla yao," alisema Kaze.

Wakati mara ya mwisho Sarpong kufunga bao ilikuwa ni Desemba 6, mwaka jana, ambapo Yanga iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Ruvu Shooting, Nchimbi hajafunga goli lolote mpaka sasa msimu huu.

Kikosi cha Yanga kinatarajia kushuka dimbani leo kuwakabili wenyeji Coastal Union, Kaze alisema anashuka kusaka ushindi tu, pia kucheza soka safi.

## Polisi Tanzania, KMC hapatoshi

**Na Shufaa Lyimo**

KATIKA kuhakikisha wanafikia malengo yao, benchi la ufundi la Polisi Tanzania limeitangazia vita timu ya KMC FC kutoka Dar es Salaam kuelekea mchezo wa Ligi Kuu Bara utakaowakutanisha leo kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, aliliambia gazeti hili kikosi chake kimefanya maandalizi mazuri na wataingia uwanjani wakifahamu ubora wa wapinzani wao.

Malale alisema wachezaji wake wako vizuri na wamejipanga kukabiliana na ushindani wowote utakaojitokeza.

"Tunaendelea vizuri na mazoezi na wachezaji wangu wanahitaji matokeo mazuri tukiwa nyumbani, tunaomba mashabiki wetu wajitokeze kwa wingi kuwapa sapoti wachezaji wetu," alisema Malale.

Kocha huyo alisema makosa madogo madogo aliyoyabaini katika michezo iliyopita ameshayafanyia kazi na anaahidi hayatajirudia katika mchezo huo ili kujiimarisha katika msimamo wa ligi.

"Kwa sasa tunapigana tusishuke daraja, na vile tunataka kuona tunamaliza katika nafasi za juu katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, tunahitaji kutimiza malengo tuliyojiwekea katika msimu huu ambao una ushindani kutokana na uimara uliofanywa na timu zote zinazoshiriki," Malale alisema.

## Taifa Jang'ombe kutimiza ndoto

**Na Hawa Abdallah, Zanzibar**

KOCHA Mkuu wa Taifa Jang'ombe, Mustafa Hassan, amesema kikosi chake kimeimarika na hakuna kitu ambacho kitawazuia kupanda daraja na kushiriki Ligi Kuu Zanzibar katika msimu ujao wa 2021/22.

Hassan alisema wamejipanga na wataendelea kupambana katika kila mchezo watakaocheza ili kutimiza malengo yao ya kupanda daraja katika msimu ujao.

Kocha huyo alisema wanafahamu mechi zote wanazocheza ni ngumu hivyo wanahitaji kuongeza umakini na utulivu. "Tumejipanga kuhakikisha tunatimiza dhamira yetu, ili kufanya kufikia malengo tunajipanga kutumia vyema michezo yetu ya uwanja wa nyumbani na hata ugenini pia ili kuondoka na alama tatu muhimu katika kila mechi," kocha huyo alisema.

Aliongeza mipango yake hivi sasa ni kuhakikisha hapotezi mchezo wowote katika mzunguko wa pili ambao kila timu imejipanga kukamilisha hesabu zake. "Huu ndio msimu wa kupandisha timu kuelekea ligi kuu, tuna kikosi kizuri chenye wachezaji vijana ambao wakizingatia maelekezo tunayowapa, tunahakika tutapanda daraja na kucheza Ligi Kuu msimu ujao," Hassan alisema.

Taifa Jang'ombe inaongoza katika msimamo wa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja ikiwa na pointi 24.

Michezo
Alhamisi Machi 4, 2021
Nipashe




## RONALDO AFUNGUKA KUPENDA MASUMBWI

HABARI UK 22



Wachezaji wa Simba wakiwa katika mazoezi ya mwisho ya timu hiyo kabla ya kuondoka nchini kuelekea Sudan kwa ajili ya mechi ya hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Merrikh itakayochezwa jijini Khartoum keshokutwa. **PICHA: MTANDAO**

## YANGA, COASTAL KUMALIZA UBISHI

**Na Saada Akida**

POINTI tatu ni maneno yanayozungumzwa na makocha wa timu mbili, Kocha wa Yanga, Cedric Kaze na Coastal Union, Juma Mgunda kuelekea katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini Tanga.

Katika mechi ya leo Yanga itawakosa nyota wake watano akiwamo Carlos Carlinhos anayetumikia adhabu ya kadi nyekundu, alionyeshwa moja kwa moja kwa kosa la kumpiga ngumi beki wa Ken Gold, Boniphace Mwanjonde wakati timu hizo zilipokutana kwenye mechi ya Kombe la FA.

Kaze alisema wachezaji wake wako tayari kwa ajili ya kutafuta pointi tatu katika mchezo huo licha ya mipango kutibuka kwa kumkosa Carlinhos.

Kocha huyo alisema kiungo huyo alikuwa katika mipango yake katika mchezo wa leo dhidi ya Coastal Union, lakini amelazimika kubadilisha mpango huo na hivyo watashuka dimbani na mbinu nyingine.

Naye Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, alisema wamejiimarisha vizuri kuhakikisha wanapata matokeo chanya na kutoipa nafasi Yanga kuondoka na pointi katika mchezo huo.

"Tumejiandaa vizuri kwa ajili ya mchezo huo, kila kitu kinaenda vizuri, tunawaheshimu Yanga kwamba ni timu kubwa na haijapoteza pointi ila kwa upande wetu tunahitaji kupata matokeo chanya katika mchezo huo ambao utatuweka sehemu salama katika msimamo wa ligi," alisema Mgunda.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo ni Polisi Tanzania dhidi ya KMC wakati Prisons wataikaribisha Mbeya City huku Biashara United ikiwafuata Mtibwa Sugar.

# GOMES AICHAMBUA AL MERRIKH

## Asema anakifahamu vyema kikosi hicho, aendelea 'kukisoma', Morrison aachwa Dar...

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

WAKATI wawakilishi wa Tanzania katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba wakiwasili salama nchini Sudan, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Didier Gomes amesema kwa sasa kazi yake kubwa ni kupitia 'mafaili' ya wapinzani wao Al Merrikh ili kufahamu ubora na udhaifu wa kikosi chao.

Al Merrikh inatarajia kuikaribisha Simba katika mechi ya Kundi A ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa keshokutwa Jumamosi jijini Khartoum.

Akizungumza na gazeti hili kabla ya kuondoka nchini, Gomes alisema anawafahamu vizuri wapinzani wao kwa sababu aliwahi kuwafundisha kabla ya kujiunga na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Gomes alisema anaimani mchezo huo wa Jumamosi utakuwa mgumu na ushindani kwa pande zote mbili kwa sababu ya kujiimarisha kwenye msimamo wa kundi hilo.

"Mechi itakuwa ngumu sana kwa sababu wenzetu wamepoteza mechi mbili za kwanza, ninaamini wakiwa nyumbani hawatahitaji kupoteza tena, ninajua hautakuwa mchezo rahisi, lakini sisi tumejipanga kwenda kutafuta matokeo chanya, tunawaheshimu wapinzani wetu tutaingia uwanjani kwa tahadhari kwa ajili ya kupambana kuhakikisha tunapata matokeo mazuri," alisema Gomes.

Kocha huyo aliongeza kama wachezaji wake wataendeleza kiwango walichokionyesha katika mechi za hivi karibuni, mchezo huo hautakuwa na ushindani na changamoto na watakuwa kwenye nafasi kubwa ya kuchukua pointi tatu.

Mfaransa huyo alimtaja mshambuliaji na nahodha wa timu hiyo, John Bocco amerejea katika ubora wake na ataendelea kumpa dakika 20 katika michezo inayofuata ili kumfanya awe imara siku zijazo huku pia hali ya afya ya golikipa chaguo la kwanza, Aishi Manula imeimarika.

"Alhamdulillah, shukrani kwa dua na sala zenu kwangu, kwani haikuwa rahisi. Ahsante kwa madaktari na wale walionipa huduma ya kwanza baada ya kupoteza fahamu pale kiwanjani," Manula ambaye aliumia katika mchezo dhidi ya JKT Tanzania alisema.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu amesema uamuzi wa kutanguliza maofisa wa timu huko Khartoum unalenga kujiweka katika usalama na itaendelea kufanya hivyo katika kila nchi watakayokwenda kupambana.

"Tulituma maofisa pamoja na baadhi ya viongozi kutoka kwenye benchi letu la ufundi wiki iliyopita na wengine waliondoka jana (juzi) kwa ajili ya kuimarisha usalama, tunajua tunakwenda vitani na lazima tujilinde, kwa kifupi tulitanguliza ujumbe," alisema Murtaza.

Aliwataja wachezaji 25 ambao wameondoka katika msafara huo kuwa ni pamoja na Manula, Beno Kakolanya, Ally Salim, Shomary Kapombe, Joash Onyango, Paschal Wawa, Erasto Nyoni, Gadiel Michael, Mohammed Hussein, Jonas Mkude, Rally Bwalya na Mzamiru Yassin.

Nyota wengine ni Luis Miquissone, Hassan Dilunga, Ibrahim Ajib, Clatous Chama, Francis Kahata, Meddie Kagere, Bocco, Tadeo Lwanga, Miraji Athumani, Chriss Mugalu, Peter Muduhwa, Kennedy Juma na David Kameta huku kiungo mshambuliaji 'mtata', Bernard Morrison akiachwa.

Simba imekwenda katika mechi hiyo ikiwa na rekodi nzuri ya kushinda michezo yake miwili iliyotangulia na kuifanya iwe kinara katika Kundi A ikifuatiwa na AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Al Ahly zenye pointi tatu kila mmoja wakati Wasudan hao wanaburuza mkia .

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042